

USHAWISHI

 Baba yetu wa Mbinguni, kwa kweli tunashukuru alasiri ya leo kwa ajili ya haya, majaliwa mengine kusimama mimbarani, kutangaza utajiri wa ajabu wa Yesu Kristo, kwa ulimwengu unaokufa bila Mungu, bila Kristo, bila tumaini, na bila tumaini la kwenda na Yesu wakati atakapokuja. Nasi tunajaribu, Bwana, kumleta Yesu Kristo kwa mataifa. Na wakati tumekusanyika hapa alasiri ya leo, jalia Roho Mtakatifu anene na kuipasha moto mioyo yetu, na kututia moyo Njiani, jalia wagonjwa waponywe na wenye dhambi waokoke, na wale waliovunjika moyo watiwe moyo. Na hebu Mungu na apokee utukufu wote na heshima, na hebu yaelekezwe kwa Jina Lake, kwa kuwa hilo ndilo kusudi letu. Kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

Ketini.

² Nina furaha alasiri ya leo kusimama hapa tena, na kuwa Beaumont. Na kwa kawaida mimi huwa mchovu. Nimekuwa nikiendelea tangu Krismasi, moja kwa moja. Si sana mahubiri ninayofanya, yanayonifanya mchovu. Ni maono ndiyo hunichosha. Bwana wetu, moja lilimfanya ageuke, na kusema nguvu Zake zilikuwa zimemtoka. Ono moja juu ya nabii, Danieli, alisema alisumbuka kichwani mwake kwa siku nyingi. Na kwa hiyo sisi—sisi hatuwezi kuyaelezea mambo hayo. Tunajua tu kwamba yako hivyo, na hakuna anayejua zaidi ya wale yaliyowafanyikia. Na kwa hiyo tuna furaha, basi. Ninachojaribu kufanya ni kutumia karama ya unabii kwa huduma ya kiinjalisti, na kamwe haifanyi kazi namna hiyo, kweli. Ni vigumu sana.

³ Kwa hiyo, ila nataka kusema hivi, nitakapofikia mwisho wa safari, na jiji hili hapa litakapoinuka, na ikiwa ninii... kizazi hiki katika siku za mwisho, si—sitaki damu ya mtu yeyote juu yangu. Ninataka niwe huru na damu yote. Nami nimejaribu niwezavyo ku—kuileta katika njia ya Kimaandiko, huduma hii ambayo Bwana amenipa, katika kila njia niyuayo. Pia ninajua kwamba Roho Mtakatifu, kwa neema Yake, hunijalia niishi hivyo, hata sidhani kumekuwa na madoa yoyote.

⁴ Ninamshukuru Ndugu Pearry Green na ndugu hawa wengine hapa ambao wametia juhudi zao kuufanya huu kuwa mkutano wa mafanikio. Iwapo kuna yeyote aliyepotea, katika jiji hili, katika kizazi hiki, hakika haitakuwa juu ya jamaa hao, kwa kuwa wamefanya kila wawezalo kujaribu kuufanya wenye ma—mafanikio. Kuwalisha watu, kuwatafutia mahali pa kulala, na—na kwenye televisheni, kila mahali, wakitoa tu fedha moja kwa moja kutoka kwa mifuko yao na kuzitoa, ili kwamba... Walijua kwamba u—u—umati tulio nao usingeweza kuunga

mkono namna hiyo, na kwa hiyo wakazitoa kwa mifuko yao wenyewe, kufanya hayo.

⁵ Basi nafikiri hilo ni zuri sana, nampenda mtu mwenye ono kama huyo. Naamini ilisemwa katika Waebrania, mlango wa 11, “Ambao ulimwengu haustahili kuwa nao.” Na kuitoa shingo yao, katika wakati ambapo hu—huduma haipendwi sana na watu wengi wanaopaswa kuiamini. Wale ambao . . .

⁶ Imenenwa habari zake, lakini, jambo fulani likitendeka, basi wanashindwa kuliona. Bali halina budi kuwa hivyo tu. I—inakubidi kuinua tu mabega yako na kuendelea na safari, ili kujua hilo. Kumbuka, kabla ya wakati wako, lilikuwa ni jambo lilo hilo. Wanapiga hatua moja kwa moja barabarani vivyo hivyo. Watu kamwe hawajawahi kuifahamu saa ya kuzuriwa kwao. Hakuna mmoja wa manabii aliyepata kujulikana.

⁷ Yesu alisema, “Mliwaweka makaburini. Mnayapaka chokaa makaburi yao sasa. Ninyi ndio mliowaweka mle. Ni yupi ambaye Mungu alimtuma ambaye hamkumtesa na kumwua?”

⁸ Hebu tuichukue kuanzia hapo na kuendelea. Tuteremke kupitia Martin Luther, na kuendelea kote, vema, Ireneo, na Mtakatifu Martin. Na kote kupitia nyakati imekuwa vivyo hivyo, hata kufikia Jona . . . Joan wa Arc, nabii mke wa Bwana.

⁹ Na enyi Wakatoliki. Wakati mwanamke huyo angeona maono, na kadhalika, na kuyasema, yangetimia tu kama alivyosema. Mlifanya nini? Mlimchoma moto kwa ajili ya dini, kuwa ni mchawi. Yapata miaka mia mbili baadaye, mliamka na kutambua kile mlichokuwa mmefanya. Hakika, walifanya vitubio, walifukua miili ya wale makasisi waliomchoma moto, na kuitupa mtoni. Hicho ni kitubio kikuu cha kufanya. Walishindwa.

¹⁰ Walisema Mtakatifu Patrick alikuwa ni Mkatoliki wa Rumi. Yeyote anayejua historia anajua kuwa hiyo si kweli. Yeye hakika, kwa uthabiti, hakukubaliana na papa. Kamwe asingeenda kuketi. . . Yeye—yeye asingeamini hayo hata kidogo. Jina lake lilikuwa ni Sucat; halikuwa Mtakatifu Patrick. Lakini alipokuwa amekufa na kuondoka, nanyi mkawaua maelfu ya watoto wake. Shule zake, asingeruhusu msalaba wa sanamu au chochote kile kuwa katika shule zake, na ingali inasimama, huko Ayalandi ya Kaskazini leo, kitu kile kile. A—asingeuruhusu huo kuingia katika shule zake. Kasema, “Watu wangekuwa wakizitazama sanamu, badala ya kile anachotaka waone.” Alikuwa na uweza wa Roho Mtakatifu. Alinena kwa lugha. Alikuwa na miujiza mikuu na ishara. Ni kwa nini kanisa lishubiri hayo leo? Mnaona?

¹¹ Na watu hao wote, kamwe hawawajui mpaka wawe wameondoka, wameaga dunia, ndipo tunajaribu kuyajenga makaburi yao. Ni kweli kwamba tunaishi katika . . .

¹² Kanisa daima linaishi katika mng'ao wa nuru ya siku nyingine. Ndipo, basi, mng'ao ni nuru bandia. Mng'ao ni nini? Ni kama mazigazi barabarani. Jua huangaza chini na kufanya mazigazi. Huonekana kama maji, bali, hayo, kamwe huwezi kuyafikia; hayako. Hivyo ndivyo watu wafanyavyo leo hii. Wanaahidi kitu ambacho kitakuwa mbali sana, ama kitu kilicho huko nyuma kabisa, ama huku juu, ila kamwe hawakifikii.

¹³ Ninashukuru sana kwamba Mungu wetu si Mungu wa namna hiyo. "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Tunalifikia tunapoliamini. Lipo pale pale, kila kitu kilichoahidiwa kwa ajili ya wakati. Hulifanya kuwa gumu, lakini hata hivyo inatubidi kuendelea vivyo hivyo moja kwa moja, tukiamini.

¹⁴ Nami hakika ninathamini ushirikiano mzuri wa wote wakati tukiwa hapa jijini.

¹⁵ Nilikuwa hapa miaka mingi sana iliyopita pamoja na rafiki yangu wa kale, Ndugu Bosworth, na Raymond Richey, na ndugu wengi waliokuja hapa. Ningali ninaiamini Injili ile ile. Sijabadilika hata kidogo; bado ni kitu kile kile tu. Lakini, mnaona, uamsho ulikuwa ukiendelea wakati ule. Na mahali ambapo hapana uamsho, huwezi kufanya mambo yatendeke.

¹⁶ Huduma imeimarika sana. Ilikuwa tu ikiwaambieni, wakati huo, hii ingekuja. Ni wangapi wanaokumbuka jambo hilo? Hakika, mnakumbuka. Nayo imekuja hasa jinsi ilivyosema ingekuja.

¹⁷ Wakati huo ningewachukua watu na kuweka mikono yangu juu yao; niliwaambieni kile Yeye alichoniambia, na hivyo ndivyo kilivyotukia. Ni hakika kabisa. Haijawahi kukosa kuwa kweli, kila wakati, kwa hiyo haina budi kutoka kwa Mungu. Hakuna mtu angalitilia hilo shaka. Bali, mnaona, uamsho hauendeleei.

¹⁸ Uwepo wenu tu, kuingia pamoja na watu, mbona, watu wangeamka kutoka kwenye vitanda vya wagonjwa na machela, na kutembea. Weka tu mikono yako juu yao, na, jamani, hiyo iliwafanya tu kufadhaika. Nimeona mistari ambapo pangekuwa na watu mia nne na mia tano wakipitia kwenye mistari, viziwi, bubu, vipofu, wenye makengeza, na hakuna hata mmoja wao anayekosa ila waliponywa, kila mmoja wao.

¹⁹ Ujaribu hiyo leo? Mnaona, hamna moto. Huko Rumi, wakati mi—mioto ilipozimika katika hekalu huko Vista, watu walienda nyumbani. Mnaona? Sasa hakuna moto wa uamsho kuuchochea, mnaona, ni, ni hayo tu.

²⁰ Baada ya kitambo kidogo, ulimwengu ukidumu, wataanza kuishi kwenye mng'ao tena. Mnaona? Na hivyo ndivyo imefanya daima, inapita na wanaikosa; na kizazi hicho kinahukumikiwa kwa sababu ya kile kilichowapita, wanakosa kukiona.

²¹ Yesu Kristo yu hai alasiri ya leo. Yeye anatembea kuzunguka hapa pamoja nasi sasa. Yeye yupo daima. "Popote

walipokusanyika wawili watatu katika Jina Langu, nipo miongoni mwao.” Mtaamini hilo, sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²² Natumai, Bwana akikawia, niweze kurudi na kuwa pamoja nanyi wakati mwingine, tena. Nisipowaona tena; nitakapokutana nanyi kule kwenye Kiti cha Hukumu cha Kristo, ambako sote tutakutana, kumbukeni, nimewaambia Kweli. Ningali nitakuwa nikisema hiyo nitakapokutana nanyi Kule. Hadi wakati huo, Bwana na awabariki, sana.

²³ Niombeeni. Ninahitaji maombi yenu. Mimi si kijana kama nilivyokuwa wakati ule. Hiyo ni karibu miaka kumi na miwili, kumi na minne iliyopita.

²⁴ Na mtu fulani aliniuliza hivi majuzi, kasema, “Una umri gani, Ndugu Branham?”

²⁵ Nikasema, “Ndiyo kwanza nipite miaka ishirini na mitano.” Nikasema, “Miaka ishirini na mitano iliyopita ni—niliupita.” Nami...huninii...U—unaweza kutambua hilo. Mtu huninii tu...

²⁶ Unapozaliwa, unaanza kukua, kama mshumaa, ama kuchomeka. Unawashwa, bali unakua mpaka unapokuwa na umri wa miaka ishirini na miwili hadi ishirini na mitatu. Sijali unajitunza vizuri jinsi gani, unaanza kufa papo hapo, na unaanza kudhoofika na kudhoofika mpaka unapokwisha.

²⁷ Niliuliza, kwenye Kiwanis siku moja nilipokuwa nikihubiri, nikasema, “Ninataka mtu fulani...”

²⁸ Daktari fulani akaniambia, kasema, “Siwezi kuiamini hadithi ya Kristo, kwa sababu siwezi kuamini kuzaliwa na bikira.” Akasema, “Siamini kuna kitu kama hicho.”

²⁹ Nikasema, “Kuzaliwa kwa kawaida hakuelezeki kwangu mimi kuliko kuzaliwa na bikira.”

³⁰ Kuzaliwa kwa kawaida, kuona jinsi kunavyofanyika, na jinsi kunavyoamuliwa, wakati hilo linachavushwa, ni yai gani, wakati kuna maelfu ya mbegu na maelfu ya mayai. Si mbili za kwanza zinazokutana, hilo latosha, lakini labda... Unasema, “Vema, kama mbili ziko mbele.” Loo, la. Unaona, itasimama. Moja labda itainuka, mbegu inayotoka huko nyuma kabisa ya mbegu za kiume, upande huu, na ya katikati ya yai inaamua kama atakuwa ni msichana au mvulana, mwenye nywele nyeusi, nywele nyekundu, macho ya bluu, ama chochote kile atakachokuwa. Kitu fulani hufanya uamuzi huo. Zingine zote zinaangamizwa.

³¹ Ni ajabu sana kuiona kazi ya Mungu, na kisha kuona watu walio na akili ndogo pungufu, kama tulivyo sisi, wakijaribu kuzikana kazi Zake kuu!

³² Jamaa huyu aliniambia, vema, yeye “asingeweza kuamini chochote ambacho hakingeweza kuthibitishwa kisayansi.”

Nikasema, “Je, unaamini una nafsi?”

Akasema, “Hakika.”

³³ Nikasema, “Basi nithibitishie kisayansi kuwa una nafsi.”
Nikasema, “U—unaamini kwamba kuna kitu kama upendo?”

Akasema, “Hakika.”

Nikasema, “Unampenda mke wako?”

“Naam.”

³⁴ Nikasema, “Basi nionyeshe, kisayansi, ni sehemu gani kwako ambayo ni upendo. Ninataka kununua baadhi yake. Nitaenda kwenye duka la dawa, popote wanapouzia huo. Ninataka huo kwa wingi. Ningependa kununua upendo kiasi.” Mnaona? Ninii. . .

³⁵ Yote silaha zote za Mungu ni za kimbinguni. Upendo, furaha, amani, uvumilivu, unyenyekevu, upole, subira, na Roho Mtakatifu. Mnaona? Kila silaha ya mwaminio ni kutazama Yasiyoonekana, kuamini yanayosemwa. Mnaona? Huoni kile unachoamini. Mnaona? Huoni. Hukioni, kwa vyovyote vile. Unakiangalia, kwa macho yako; unaona kwa moyo wako. Mnaona? Unaangalia kitu chochote, unasema, “Sikioni kabisa,” unamaanisha hukielewi. Mnaona?

³⁶ Kwa hiyo nikamwuliza hili, nikasema, “Kama ningalikuwa na jagi ya maji, na niweke bilauri hapa. Nami ninamimina maji kutoka kwenye jagi hii, katika bilauri hiyo, na ijae nusu; ndipo basi niendeleo kumimina maji, halafu ianze kupungua. Kisayansi niambie yanakoenda hayo maji.” Mnaona?

³⁷ Nikasema, “Nilipokuwa mvulana mdogo, umri wa miaka kumi na sita, nilikula chakula kile kile ninachokula sasa, maharagwe, mkate, viazi, nyama.” Nikasema, “Kila mara ninapokula, kilifanya nini? Kilijenga seli za damu. Nilikuwa mkubwa zaidi na mwenye nguvu zaidi, kila mara, na nilipofikisha yapata umri wa miaka ishirini na miwili. Ninakula zaidi na bora sasa kuliko nilivyokula wakati huo, maana sikuwa nacho wakati ule kula. Bali ninakula zaidi na bora kuliko nilivyofanya, sasa ninazidi kuzeeka na kuwa mnyonge zaidi. Na, hata hivyo, chakula hicho kinajenga seli za damu. Ninaongeza uhai mpya kila mara, na kuzidi kudhoofika kila mara.” Ni miadi. Tutaitimiza, hiyo ni pamoja na Mungu. Hiyo ni kweli. Itatubidi kuitimiza.

³⁸ Huwezi kumthibitisha Mungu kisayansi. Unamwamini tu Mungu, na unamwamini kulingana na Neno Lake.

³⁹ Sasa, alasiri ya leo, ninataka kumshukuru kila mmoja wenu. Maskini dada mzuri pale kwenye pi—piano, huyu hapa. Nanyi watu wote, wahudumu, kila mmoja wenu, Bwana awabariki.

⁴⁰ Usiku hautakuwa na giza kupita kiasi, mvua haitanyesha kupita kiasi, ila kile ningaliwasaidia kama ningaliweza.

Nilikuwa nikisema ningeweza kuja kwenu, bali kuna wengi sana sasa. Ni, nimekuwa ulimwenguni kote, mnaona, na ni kila mahali. Lakini nipigie tu simu, au uniandikie barua; nitakutumia kitambaa cha maombi, chochote niwezacho kufanya, kila kitu bila malipo hata kidogo. Hakuna fedha katika hili. Mnaona? Ninii. . .

⁴¹ Nilidumisha mikutano yangu hivi kusudi niweze kuja mahali ambapo hawana fedha zozote. Nilifanya mkutano, hapa si muda mrefu uliopita, katika ma—maskani iliyokuwa tu na watu ishirini, mkutano wa siku mbili usiku. Ilikuwa mbaya sana, chini yapata kumi chini ya sufuri, bali Bwana alinituma huko na mambo makuu yalitendeka.

⁴² Sina—sina vipindi vikubwa, redio, televisheni, mambo haya mengine yote. Ndugu wengine wana hayo. Wao labda wana akili, watu walioelimika. Wanajua la kufanya, na Bwana analijalia. Kama, Oral Roberts, na mtu kama huyo ambaye inambidi kuwa na maelfu ya dola kila siku, hawezi kutenda kazi vyovyote vingine; na hilo ni kwa kusudi jema. Na hiyo si yangu.

⁴³ Niliitaka yangu ibaki kuwa ndogo na nyenyekevu, popote niwezapo kwenda, na popote Mungu aniitapo. Sina kitu cha kunizuia basi. Ninaondoka tu na kwenda popote palipo. Hiyo ndiyo huduma yangu.

⁴⁴ Niombeeni, ya kwamba Bwana atanisaidia kudumisha Imani, wala nisiangalie nyuma; niangalie mbele ninakoenda. Si kuangalia kule nimekuwa; kuangalia ninakoenda. “Tukisahau yale mambo yaliyopita, tunakaza mwendo tuifikie mede ya mwito mkuu katika Kristo.”

⁴⁵ Ninataka kusoma baadhi kutoka kwa Biblia ya Mungu, leo. Nimechagua fungu dogo tu, maana niliwaambia ningekuwa huku na kuwaombea wagonjwa alasiri ya leo. Wale wote walio na kadi za maombi, na wale wanaotaka kuombewa, wataombewa. Tutafanya hivyo. Nami daima hujaribu kutimiza ahadi yangu.

⁴⁶ Sasa, mtu fulani, unaposema hilo, anasema, “Vema, uliahidi kuwa mahali fulani.”

⁴⁷ Nisingetilia shaka ila kuna sehemu nne au tano katika Marekani papa hapa, ninazopaswa kuwako leo hii, ambako mtu fulani alisema ningekuwa huko. Sikusema ningekuwa huko. Lakini wao wanasema, mnaona, wakaliweka kwenye gazeti. Nao wanapiga simu nyumbani, kila mara, “Vema, kuna shida gani?” Wanamwambia mke wangu, ama baadhi ya wafanya kazi wa ofisini, “Vema, alipaswa kuwa hapa. Walimtangaza hapa. Vema, tangazo hilo liko kwenye gazeti.” Hata sikujua chochote kuhusu hayo. Siwezi kusaidia hayo. Ninawajibika tu kwa yale ninayosema, mwenyewe.

⁴⁸ Kwa hiyo sasa, alasiri ya leo, ninataka sisi sote, tena, kama tunaweza, tusimame kwa ajili ya kusomwa kwa Neno.

49 Nasi tutajaribu kuondoka katika saa nyingine moja, Bwana akipenda, ili mweze kuwa na nguvu kwenda kanisani usiku wa leo. Na sababu ya sisi kuwa na mikutano hii Jumapili alasiri, tusije tukawanyang'anya yeyote kutoka makanisani mwenu. Watu wanaotaka kuombewa hapa, wagonjwa na wanaoteseka, vema, daima sisi hupata kuwaombea, basi haikatizi ibada yenu.

50 Haijalishi, kuna mara nyingi kuna mtu ambaye si... sikubaliani naye, nao hawakubaliani nami. Lakini kama haiwezi kuwa juu ya uvumilivu, na juu ya mawazo ya ushirika bora na kadhalika, basi si—sitasema lolote juu yake. Kama ninaweza kukosa kukubaliana na mtu, sana, ikiwa siwezi kumkumbatia na, kutoka moyoni mwangu, nijue yeye ni ndugu yangu, basi sipaswi kuwa nikizungumza naye. Hiyo ni kweli. Inatupasa kufanya hivyo.

51 Sasa ninyi mnaotaka kufungua kwenye Biblia zenu, fungueni Isaya, mlango wa 6. Ninataka kusoma kutoka hapo alasiri ya leo, kwa ajili ya ibada ya kufunga, nichukue somo.

Katika mwaka ule...aliokufa Uzia nalimwona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana na kuinuliwa sana, na pindo za vazi lake zikalijaza hekalu.

Juu yake walisimama maserafi; kila mmoja... alikuwa na mabawa sita; kwa mawili alifunika uso wake, na kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka.

Wakaitana, kila mmoja na mwenzake, wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni BWANA Mungu wa majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake.

Na misingi ya vizingiti ikatikisika kwa sababu ya sauti yake aliyelia, nayo nyumba ikajaa moshi.

Ndipo niliposema, Ole wangu! Kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu; na macho yangu yamemwona Mfalme, BWANA wa majeshi.

Kisha mmoja wa maserafi wale akaruka akanikaribia; naye alikuwa na kaa la moto mkononi mwake, ambalo alikuwa amelitwaa kwa makoleo toka juu ya madhabahu;

Akanigusa kinywa changu kwa kaa hilo, akaniambia, Tazama, hili limekugusa midomo yako, na uovu wako umeondolewa, na dhambi yako imefunikwa.

Kisha nikaisikia sauti ya Bwana, ikisema, Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi.

52 Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

⁵³ Bwana Mwenye neema nyingi, yachukue maneno haya, na jalia tafakuri ya moyo wetu sasa ikubalike Kwako. Jalia Roho Mtakatifu mkuu aingie kwenye midomo ya mnenaji na masikio ya msikilizaji, kwamba pamoja iweze kuleta heshima kwa Jina Lako, kupitia Neno Lako, kwa kuwa tunaomba hayo kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

Mwaweza kuketi.

⁵⁴ Ninaenda kuangalia sasa, kile, kusudi tuweze kuwa na muda mwingi kwa ibada ya uponyaji. Sasa sikilizeni kwa makini ninapojaribu, pamoja na haya Maandiko machache na muhtasari nilioandika hapa, kulizungumza. Wakati mwingine, mimi sijachoka na kuisha kabisa, (ambapo) siandiki chini Maandiko, nikijua ninaweza kuyakumbuka. Lakini siku hizi imekuwa tu hivi wakati mwingine ninasa-...siwezi kuyakumbuka. Kwa hiyo ninayaandika tu hapa, ki-kitu kidogo kama Maandiko fulani, ninajua hicho kinachomaanisha, nami ninaanzia tu hapo na kuendelea.

⁵⁵ Ninataka kuzungumza juu ya somo la: *Ushawishi*.

⁵⁶ Sasa, mnajua, yupo mtu unayemshawishi. Maisha yako ni waraka ulioandikwa unaosomwa na watu wote. Hivyo basi, ikiwa maisha yako si kulingana na ushuhuda wako, au ushuhuda wako kulingana na maisha yako, hasa, basi kuna...unaweka jiwe la kikwazo njiani mwa mtu fulani, kwani mtu fulani anakuangalia. Maskini mtoto fulani anamwangalia mama yake, anamwangalia baba yake.

⁵⁷ Miaka fulani iliyopita, nilisoma makala fupi, mnamo wakati wa Krismasi, iliyokuwa...kweli iliuchochea moyo wangu, ilikuwa ni huzuni. Wakati ja—ja—jamaa fulani alikuwa amekuwa nje, naye alikuwa ni mtu mwema, hakuninii—hakunywa pombe, kabisa. Lakini a—alikuwa amekuwa nje, msimu wa Krismasi, akiwatembelea wenzake, na wote wakamwambia, kasema, “Yohana, onja kidogo, kinywaji kidogo tu,” na kutoka nyumba moja hadi nyingine a—alikuwa kupindukia. Ndipo ilimbidi kurudi nyumbani. Basi akipitia kwenye uwanja, mvulana wake mdogo alikuwa pamoja naye, ndipo a—akamkosa mvulana huyo mdogo. Kisha akageuka na kuangalia, naye mvulana huyo mdogo alikuwa tu akitoka upande mmoja hadi mwingine. Naye baba akangojea mpaka mvulana huyo mdogo akamfikia.

⁵⁸ Akasema, “Kwa nini unaenda kote uwanjani, mwanangu? Ni kitu gani kinachokufanya kutembea namna hiyo?”

⁵⁹ Akasema, “Baba, ninajaribu kufuata nyayo zako.” Na hiyo ni kweli. Mnaona? Maskini... .

⁶⁰ Mtu huyo akamchukua maskini mvulana huyo, akaketi chini, akamkumbatia huyo jamaa mdogo. Akasema, “Mungu, nisamehe. Ninataka kutembea sawa, ili mwanangu nyuma yangu atatembea sawa.”

⁶¹ Na hilo ndilo tunalotaka kufanya, kama Wakristo. Tunataka kutembea kama Wakristo, kuishi kama Wakristo, kuongea kama Wakristo.

⁶² Miaka mingi iliyopita, walipokuwa na utumwa huko Kusini, hao huko chini Kentucky na Alabama, na huko chini ninakotoka. Walikuwa wakiwachukua Waafrika na kuwanadi, kwenye—kwenye jengo la mnada, kama vile tu ungekuwa na motokaa za mtumba au kitu kingine. Ninaamini hakuna mtu anayepaswa kuwa mtumwa. “Mungu alimwumba mwanadamu, naye mwanadamu akafanya watumwa.” Nao walikuwa wakija pale na kuwanunua, kama vile tu ungenunua motokaa ya mtumba, upate stakabadhi, na kadhalika. Hilo lilikuwa jambo baya sana.

⁶³ Kwa hiyo wao, siku moja, kulikuwa na mnunuzi aliyekuja kuninii . . . dalali, kwenye shamba la kale lililokuwa na watumwa wengi. Naye akasema, “Una watumwa wangapi?”

“Loo,” kasema, “karibu mia moja na hamsini huko nje, nadhani.”

Kasema, “Je! ninaweza kwenda huko nje niwaangalie?”

Akasema, “Hakika, jihudumie.”

⁶⁴ Kwa hiyo akatoka nje kuwaangalia wa—watumwa. Ndipo alipoangalia kote, aliwaona jamaa hao, daima walikuwa na huzuni. Hao, Makaburu, waliwaleta kutoka Afrika na kuwashusha huko Kuba, na kisha wakawatuma huko Kusini na kuwauza kuwa watumwa. Nao walijua hawatawahi kurudi nyumbani. Wanajua kwamba kamwe hawataona baba yao na mama, tena, au watoto wao, mume, wake, na kadhalika. Walikuwa—walikuwa wanateseka kutokana na hali ambayo hawakujiletea wenyewe. Na hapa walikuwa, mbali na nyumbani, na wamehuzunika. Na wakati mwingine ingewabidi kuchukua mijeledi na kuwacharaza, kama tu wanavyomcharaza mnyama, ng’ombe, na maksai, farasi, na kadhalika, na kisha wa—wanawafanyiza kazi.

⁶⁵ Na hili waliona, dalali huyu kijana aliona kulikuwa na mmoja wa hao watumwa vijana ambaye haikuwabidi kumcharaza. Jamani, alikuwa amekiinua kidevu chake, mabega yake nyuma, naye alikuwa tayari kabisa kila wakati. Haikuwabidi kumfanyia chochote. [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] Alitekeleza wajibu. Kwa hiyo mwenye watumwa akasema . . . Dalali huyo akamwambia huyu bwana mwenye shamba, kasema, “Ningependa kumnunua yule mtumwa.”

Akasema, “Loo, hapana.” Kasema, “Huyo si wa kuuzwa.”

⁶⁶ Akasema, “Vema, ni kwa nini yeye hauzwi?” Kasema, “Ni kitu gani wewe,” kasema, “ni kitu gani wewe . . . Ni nini

kinachomfanya kuwa hivyo?” Kasema, “Je! yeye ndiye boshi wa hao wengine?”

Kasema, “Loo, la. Yeye ni mtumwa.”

Kasema, “Hivi huwa unamlisha tofauti na unavyowalisha hao wengine?”

⁶⁷ Akasema, “La, wote walikula huko nje manchani, pamoja.” Kasema, “Yeye ni mtumwa tu.”

⁶⁸ Akasema, “Vema, ni kitu gani kinachomfanya kujiadhibisha tofauti na hao wengine?”

⁶⁹ Kasema, “Unajua, nilishangaa hivyo, pia, mpaka nikagundua kwamba katika nchi ya wenyeji wao, huko Afrika wanakotoka, baba yake ndiye mfalme wa kabila. Na, ingawa, yeye ni mgeni, mbali na nyumbani kwao, lakini anajua kuwa yeye ni mwana wa mfalme, naye huenenda hivyo.” Loo, jamani!

⁷⁰ Wakristo wanapaswa kufanya nini? Sisi ni wana na binti za Mfalme. Ingawa tu wageni, hebu tuenende kama wana na binti. Wanawake, acheni nywele zenu zikue. Acheni kuvaa hayo mavazi mnyavaa, ya kizinifu na kadhalika. Wanaume, rudini mahali mwanamume anapaswa kuwa. Msininii . . . Tendeni kama wana na binti za Mungu. Wewe ni mgeni hapa, bali, kumbuka, sisi ni wana wa Mfalme.

⁷¹ Angalia ushawishi ambao mtu huyo alikuwa nao juu ya hao wengine, uadilifu wake uliina matumaini ya hao wengine.

⁷² Tunaona kwamba huyu mfalme, Uzia, alikuwa kijana mchungaji katika siku za Isaya, nabii. Isaya alikuwa nabii.

⁷³ Manabii wanazaliwa. Hao si kuwawekea tu mikono, na kuwafanya manabii. Wanazaliwa, wamekusudiwa kimbele na Mungu. “Karama na miito havina majuto.” Kuna ka—karama ya unabii kanisani, nayo haina budi kuamuliwa na watu watatu kabla ya sauti hiyo kuwahi kusikika miongoni mwa kusanyiko, lakini hiyo ni karama tu ya unabii. Bali nabii amekusudiwa pamoja na BWANA ASEMA HIVI, tangu utotoni akikua.

⁷⁴ Naye Isaya alikuwa nabii wa Bwana, na alikuwa amepolekwa hekaluni. Ndipo alikuwa na . . . Huyu Uzia, huyu mvulana mdogo mchungaji, alikuwa u—ushawishi mkubwa juu ya nabii huyu kijana. Kwa sababu, Uzia, katika Mambo Ya Nyakati ya Pili 26, inatwambia kwamba alikuwa amefanyika mfalme wa Israeli wakati akiwa tu na umri wa miaka kumi na sita. Baba yake Amazia alikufa, naye akachukua mahali pake, kutawala, kama ilivyokuwa desturi kwamba mwa—mwana alimrithi m—mfalme. Nao walimchukua na kumfanya mfalme alipokuwa tu na umri wa miaka kumi na sita. Na alikuwa na baba yake, Uzia . . . Amazia alikuwa ni—alikuwa ni mtu mashuhuri. Alikuwa ni mtu m—m—mcha Mungu. Na akiwa na huyu mzazi mtauwa, vema, ilimfanya kutenda yaliyo mema, kwa kuwa alishawishiwa na baba yake. Mnaona?

⁷⁵ Leo hii, unawezaje kutarajia ila kwamba hatutakuwa na wengi wa kina Oswald na kina Jack Ruby. Angalia kwenye... Nilitoka kwenye moteli yangu, muda mfupi uliopita, na machafuko ya ulevi wa kundi la Wakalifonia huko nje, wamelala pale, wanawake wamevuliwa uchi kwenye huo, huko nje wakiwa na ukanda mdogo tu waliojifunga, ama kitu kingine, huko nje. Nao wanaume wakinywa wiski kwenye—kwenye barafu na kadhalika, na kufanya yasiyofaa, wakianguka karibu na vidimbwi. Unawezaje kuwatarajia watoto wao, wachanga hapo barazani, wakicheza, kuwa chochote ila Oswald ama kitu kama hicho? Ni ushawishi uliowekwa mbele yao.

⁷⁶ Loo, Marekani imeoza kabisa. Litavuna lilichopanda. Mungu mwenye haki hawezi kuliacha liepuke na chochote kingine.

Unasema, “Je, wewe ni Mma- . . .

⁷⁷ Mimi, hakika, ni Mmarekani. Uwanjani, huko Ujerumani na Japan, yapo makaburi ya Kimarekani yaliyotiwa alama kote—kote kule, watu wangu, wa Branham. Na kama ikinibidi kuondoka, ningetoa uhai wangu kwa ajili yake.

⁷⁸ Lakini hebu niwaambieni jambo fulani. Tunahitaji kutikiswa, taifa hili linahitaji. Mambo tuliyokuwa nayo wakati mmoja, tumeyapoteza, na tunajaribu kuishi juu ya sifa ya kile mtu mwingine alifanya. Tutavuna kwa sababu ya hilo. Mungu aliifanya Israeli, watu walioupendeza moyo Wake; aliwafanya kuvuna. Nasi tutavuna, pia, kwa yale tuyafanyayo. Hatuna kitu kingine chochote mbele yetu, ila kuvuna. Tumeuvuka mstari wa neema na rehema, na hakuna kitu kingine kilichosalia ila kuvuna. Iandikeni hiyo katika Biblia zenu. Mimi ni mzee. Lakini nyinyi andikeni hilo chini na mchunguze kuona kama hilo ni kweli au la. Pengine nitakapokuwa nimeondoka, na kuendelea na kuendelea, mtagundua kwamba maneno hayo ni kweli. Tatalipata. Tumepimwa kwenye mizani na kupatikana tumepungukiwa, na hakuna njia yoyote. Hiyo ni kweli. Tayari tumeupita huo mstari. Inakubidi kuvuna ulichopanda, kila wakati.

⁷⁹ Kwa hiyo jamaa huyu kijana alikuwa ni ushawishi mkubwa juu ya huyu, mfalme kijana alikuwa ni ushawishi juu ya—juu ya nabii kijana. Naye aliegemea kwenye mkono wa nabii huyu, kwa sababu kwamba a—alijua alikuwa ni nabii. Na alikuwa naye moja kwa moja pamoja naye kila wakati, na ku—kutoa ushawishi wake kutoka kwa maono yake, na kadhalika, kutoka kwa Mungu, kujua jinsi ya kuendesha ufalme wake.

⁸⁰ Hiyo ilimfanya kuwa mtu mashuhuri. Alipuuza siasa za siku hiyo, na maoni maarufu, na kumtumikia Mungu kwa moyo mkunjufu. Huyu ndiye aina ya rais tunayemhitaji. Huyu ndiye aina ya ki—kiongozi tunayemhitaji kuongoza watu wa taifa lolote, mahali popote. Ufalme wake ulikuwa wa karibu na wa

Sulemani. Hakukuwa na kitu... Mungu alimbariki kabisa na hakumzuilia baraka yoyote, maana alimtumikia Yeye.

⁸¹ Na huu ulikuwa msaada mkuu kwa kijana Isaya, kwa kuwa aliona vile Mungu angewabariki wale walio watiifu kwa Neno Lake. Haijalishi jinsi ilivyokuwa vigumu, dumu mwaminifu kwa Neno hilo. Basi ni mfano leo hii, pia, kwetu, kubaki waaminifu kwa Neno. Nayo ilikuwa na ushawishi mkubwa juu yake.

⁸² Sasa, alipanda mashamba ya mizabibu, naye alikuwa ni mchungaji, na alikuwa na kila namna ya mifugo na mashamba ya mizabibu. Iwapo unataka kusoma, katika Mambo Ya Nyakati ya pili 26 pale, na sehemu mbalimbali za Maandiko, zinazozungumza juu ya—juu ya Uzia. Alikuwa ni mtu mashuhuri. A—alipenda shunguli za nje, na, jamaa mzuri sana! Mungu alibariki kila alichofanya. Kilisitawi tu na kuendelea. Wala hakuna mataifa yaliyomsumbua. Walimwogopa, na kwa sababu alimtumikia Bwana Mungu aliyekuwa pamoja naye; si kwa sababu waliogopa nguvu zake za kijeshi, bali walimwogopa Mungu aliyemtumikia.

⁸³ Hiyo yapaswa kuwa ndiyo kumbukumbu yetu. “Mungu wetu tunamtumaini,” inasema kwenye dola zetu, bali mimi hushangaa wakati mwingine.

⁸⁴ Sasa, lakini haya yote yalitendeka, na yanaonyesha hapa mfano. Ningependa kutoa kwenye huu, alasiri ya leo, kuonyesha jinsi ambavyo Mungu anaweza kumbariki mtu na—na kumfanya mtu mashuhuri. Bali, mnajua, wakati mfalme huyu aliponinii... alipojihisi salama, akajihisi kufikia mahali ambapo—ambapo alikuwa ameimarika tu kabisa, na hakukuwa na njia kamwe kwake kuanguka, akajikweza kwa kiburi. Hapo ndipo alipoangukia. Hapo ndipo mtu yeyote atakapoangukia.

⁸⁵ Nafikiri hiyo ndiyo shida ya wengi wa watu wetu leo, tunajikweza. Nafikiri hiyo ndiyo huyafanya madhehebu kufanya yale wafanyayo. Wanalo tabaka lililo bora, la kile wanachokiita, “tabaka bora, la watu wenye elimu nyingi,” wanavyofikiria. Watu, ninii zao... wahudumu wao wote wakiwa na elimu ya shule ya sekondari na vyuo, miaka miwili au mitatu ya saikolojia, wanawapa jaribio la akili na mawimbi ya ubongo, na kila kitu, kuona ikiwa wanafaa, na wakati mwingine hawajui chochote kuhusu Mungu kuliko sungura anavyojua kuhusu viatu vya theluji. Hiyo ni kweli. Kweli. Haya mambo ya kiakili hayana uhusiano nalo. Ni uweza wa Roho Mtakatifu. Haupo akilini mwako; umo moyoni mwako. Kweli. Bali, unaona, tunapata... Ndipo wanajikweza, “Ninii yetu, sisi huenda kwenye kanisa zuri kuliko yote jijini. Sisi ni wafuasi wa kanisa la kwanza. Sisi ni washiriki mahali meya huenda. Sisi ni wafuasi wa hili.”

⁸⁶ Na mambo haya yote pale, mnaona, kilicho, ndipo watu kwa urahisi hawawezi kusimama kusikia Hilo. Wanafikiri tu kwamba wewe ni—ni mtu wa kutisha. Bali, jambo ni kwamba,

hakuna mahali kwa ajili ya Mbegu kutulia. Hakuna kitu kwa ajili ya Hiyo kukalia juu; ni jiwe tu. Haitashikilia. “Ndege wataruka karibu na kuichukua,” Biblia ilisema.

⁸⁷ Lakini mfalme huyu alipojikweza, na kujihisi salama, alijawa na kiburi.

⁸⁸ Ninatambua, mara nyingi, tunaona hata watu, wainjilisti, wanafikia mahali ambapo wengi wao wamelaumiwa kwa mambo, na labda baadhi yake ni kweli, kunywa pombe, na kadhalika. Jambo ni kwamba, nafikiri wanajijengea ufalme mdogo, na kudhanja watu wanawapenda sana, hakuna njia yoyote kwa... Hao watu, wanaweza tu kufanya chochote watakacho, na, “Watu hao hawatajali.”

⁸⁹ Watu huenda wasijali, lakini vipi kuhusu Mungu? Hapo ndipo tunaposhindwa kuona. Ni Mungu Ndiye anayeangalia. Mnaona? Mungu anajua. Unapooa Kweli na Nuru, na kuikataa, Mungu anajua ulichofanya. Kamwe hutasonga popote mpaka urudi moja kwa moja mahali hapo tena. Huwezi kuvuka hiyo. Huna budi kurudi moja kwa moja mahali ulipoachia.

⁹⁰ Alijikweza sana moyoni mwake, na—na kujisikia salama sana na kila kitu, sana, hata akajaribu kupachukua mahali pa mhudumu. Alijaribu kuingia na kutoa uvumba, kama tunavyojua katika Biblia, kufukiza uvumba, ambayo ilikuwa tu ni kwa ajili ya Mlawi kufanya, kuhani aliyetiwa upako kwa ajili ya kazi hiyo. Alijaribu kupachukua mahali pake.

⁹¹ Na hapa tunao ushawishi wa mfalme huyu, kuwafanya watu wajue kwamba uigaji huu wa kimwili wa mmoja kwa mwingine, leo hii, si wa Bwana. Hujakusudiwa mambo kama hayo. Kamwe hutachukua mahali pa mtu mwingine, wala na mtu mwingine hawezi kupachukua mahali pako. Tafuta palipo mahali pako na udumu hapo. Unaona?

⁹² Aliwaza, “Vema, sasa mimi... Mungu asifiwe, mimi ni mfalme, naye Bwana amekuwa mwema kwangu. Ninaweza kufanya *hili*. Nina *hiki*. *Hii* ni huduma yangu.” Ndipo akaja kugundua, kwamba, katika kuendelea kwake namna hiyo, na kujaribu kuvuka, na kuvuka kile Mungu alichokuwa anambarikia.

Kama wewe ni mshiriki mwema wa kanisa, kuwa mshiriki mwema.

⁹³ Ikiwa wewe ni mke mwema nyumbani, kama Mungu amekubariki kama mke nyumbani na kukufanya mtiifu na mwaminifu, dada, wewe endelea tu kuwa hivyo. Usianze kuwazia, wewe, Mungu alikuwa kuwa mhubiri, ama—ama shemasi, ama chochote kingine.

⁹⁴ Na—nawe fanya vivyo hivyo, ewe mwanaume. Popote alipokubariki Mungu, dumu hapo, maana hapo ndipo Yeye

amekuweka. Wewe fanya tu kile anachokuambia ufanye, na uone ambapo Yeye anakubariki.

⁹⁵ Ila, usijaribu kamwe kuingia, hiyo ni—hiyo ni misingi ya Pentekoste. Wakati Bibi McPherson... Nilipokuwa nikisoma kitabu chake, sikuninii... Sikuwa mhudumu katika siku zake. Nao walisema, “Wakati angejitokeza jukwaani akiwa na haya, kama mabawa, wajua,” ama, wajua, namna ya joho kama hilo, “kila mwanamke mhubiri alivalia kitu kile kile. Kila mmoja wao alibeba Biblia kama Bibi McPherson.”

⁹⁶ Je! mliwahi kusikiliza hivi vipindi vya redio? Kila mtu, “Mungu akubariki, vizuri kabisa, ewe jamaa,” Billy Graham mwingine. Ni uigizaji wa kimwili.

⁹⁷ Nilikuwa nikisoma hi—historia ya Martin Luther. Nayo historia hiyo ilisema, “Haikuwa ajabu kwamba Martin Luther angeweza kuliiasi kanisa Katoliki na kuepuka nao, bali kusimama imara juu ya ushupavu wote wa kidini uliofuata uamsho wake.” Hiyo ni kweli.

⁹⁸ Jiweke safi na wazi, kwa wito wako. Dumu na Neno la Mungu wala usisogee kwa chochote. Halafu ukae, udumu katika wito wako. Kama akikupa kazi huko nje, kama mkulima, lima vizuri. Mungu akubariki katika hiyo, na utoe zaka zako na chochote kile, sadaka zako, kuisaidia huduma iendelee. Kama alikufanya makanika, kakubariki katika kazi hiyo, dumu nayo na umshukuru kwa ajili yake. Unaona? Wewe dumu tu pale alipokuita Mungu.

⁹⁹ Tunapata hapa ushawishi. Na ndipo alipojaribu kurekebisha, mhudumu alimfuatilia, na kusema, “Aisee! Ngoja kidogo! Wewe hukuitiwa hiyo.” Loo, akakasirika! Mbona, alikuwa tayari kukatwa kichwa.

¹⁰⁰ Mnaona, lipo jambo jingine litupasalo kujua. Haijalishi Mungu amekubariki kiasi gani, huna haki yoyote kumkemea mtiwa mafuta wa Bwana, wala kusema lolote dhidi yao. Hiyo ni kweli. Mungu ndiye anayepaswa kulishughulikia hilo. Wakihitaji kemeo lolote, hao ni watoto Wake, wewe achana nao. Hupaswi kufanya hivyo. Unaona?

¹⁰¹ Na unapo—unapowaambia watu kuhusu dhambi zao, na kuwaambia wanafanya makosa, “Ondokeni kwake! Msijaribu tu kwenda Mbinguni juu ya mfumo wa kidhehebu ama kitu kingine.” Jamani, masalaale, wangeweza, wataninii... Wanataka kupasuka. Watapasuka. Wanataka kukulalamikia; hata hawata—hawataketi na kukusikiliza; wanainuka na kuondoka, na wenye tabia mbaya, huku wakitenda vyovyote. Mnaona, hiyo inaonyesha, kwanza kabisa, malezi mabaya, maadili ya nyumbani. Hakika inaonyesha.

¹⁰² Lakini tunaona kwamba jamaa huyu alikuwa amechukua msimamo huu katika kufanya kile alichofanya. Alipatwa na nini? Bwana alimpiga kwa ukoma, mumo humo jengoni.

Nao ukoma ni mfano wa nini? Dhambi, kutokuamini. Hakuna dhambi nyingine ila kutokuamini. “Yeye asiyeamini amehukumiwa tayari.” Na dhambi ndiyo kutokuamini pekee kulikopo.

¹⁰³ Nilikuwa nikihubiri wakati mmoja katika kanisa la Methodist, ndipo nikasema, “Kuvuta sigara si dhambi. Kufanya uzinzi si dhambi. Kulichukua Jina la Bwana si dhambi.”

¹⁰⁴ Imekiuka mpaka kwa dada mmoja; akasimama, kasema, “Naomba uniambie, Kasisi Branham, dhambi ni nini?”

Nikasema, “Kutokuamini.”

¹⁰⁵ Unafanya mambo hayo kwa sababu huamini. Hiyo ni kweli. Sababu ya wewe kukataa kutembea kwenye Nuru ya Neno ni kwa kuwa huliamini Neno. Hiyo inakufanya asiyeamini.

¹⁰⁶ Jamaa fulani aliniambia, kasema, “Sijali ni visa vingapi ungeweza kuonyesha, na ni visa vingapi daktari angeweza kuonyesha, ya uponyaji mbalimbali,” kasema, “siamini uponyaji. Si kweli.”

¹⁰⁷ Nikasema, “Hakika, haukutumwa kwa wasioamini. Ulitumwa tu kwa wale wanaoamini.”

¹⁰⁸ Ni kwa waaminio pekee. Alisema, “Yeye aaminiye, mambo yote yanawezekana,” si yule asiyeamini.

¹⁰⁹ Na chembe ndogo tu ya kutokuamini dhidi ya Neno la Mungu, nawe utakaa nje ya Ufalme wa Mbingu. Kulimtoa Hawa nje. Kulisababisha taabu hizi zote, kulipotosha tu kidogo Neno mara moja. Huna budi kudumu moja kwa moja Nalo, kile lisemacho.

¹¹⁰ Sasa tunaona, mtu huyu alijawa na kiburi na majivuno, ndipo uso wake ukawa mwekundu, kisha akageuka na kuwaambia hao makuhani, na, muda si muda mwajua, akashikwa na ukoma. Papo hapo katika hasira yake, alipigwa. Kamwe hakuuondokea. Nini? Kutokuliamini Neno la Mungu alilokuwa akijaribu kuambiwa.

¹¹¹ Kuna mfano halisi katika hilo. Angalia. Yeye alikuwa... Hakuamini, na, katika hasira yake, alipigwa na ukoma; akafa, huko katika boma lake mwenyewe, hakuruhusiwa kwenye ufalme tena, mahali pa mfalme. Ilibidi mwanawe kuchukua mahali pake na—na kusaidia kadiri walivyoweza, naye aliachwa hivyo hadi alipofariki. Sasa, unaona, hakupona kamwe.

¹¹² Yesu alisema, “Neno moja dhidi Yake halitasamehewa,” Neno, “si katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao.” Ni isiyosamehewa. Basi mnaona ni kwa nini ulimwengu uko tayari kwa hukumu? Wainjilisti mashuhuri na kadhalika walioijaza dunia na Injili, wamechekwa, wakadhihakiwa, chochote kingine. Hakuna kilichosalia. Hakuna njia kwake kuwahi kurudi. Wamemkufuru Roho Mtakatifu, na kumdhihaki, na kila kitu kingine. Nao wame... Na, wao, hakuna njia kwa huo

kuwahi kurudi. Hauna budi kulipiwa. Hakuna njia ya kutoka kwa huo. Mungu ni mwenye haki; ingeenda kinyume na haki Yake, uwe kinyume na Utu Wa—Wa—Wake, kile alichu. Na sasa haina budi kulipiwa.

¹¹³ Kwa hiyo mfalme huyu, haijalishi Mungu alimpenda kiasi gani, jinsi alivyokuwa mtu mashuhuri, ni digrii ngapi alizokuwa nazo, hata hivyo alifanya makosa naye ilimbidi kuvuna alichopanda. Na kila mtu atafanya hivyo.

¹¹⁴ Hapo kukawa na somo kwa nabii huyu kijana. Hapo palikuwa na somo halisi! Kwa hili, Isaya alitambua kwamba Mungu huweka mtu wake mahali pake, Mwenyewe. Si yale mtu mwingine anayoamua. Mungu humweka mtu Wake kazini, sasa, humweka mahali pake. Haimpasi kujaribu kuchukua mahali pa mwingine.

¹¹⁵ Lile ono, kitu hicho kilikuwa kikuu sana hata kikampeleka nabii huyu hekaluni, kuomba.

¹¹⁶ Nashangaa, leo, kama tungeona kifo cha makanisa, kuona ku—kufa kwa watu, kutoka kwa Roho, wakirudi nyuma na kutumikia kanuni zao za imani, kama haipaswi kuwaweka waaminio magotini mwao.

¹¹⁷ Ilimfanya mwaminio halisi, mwaminio aliyewekwa wakfu, Isaya nabii, aende magotini mwake. Alienda hekaluni, na hapo akaanza kuomba.

¹¹⁸ Ndipo, hekaluni, akamwona Mungu juu ya kiti Chake cha enzi, ameinuliwa juu kabisa. Mungu alikuwa anaenda kumwonyesha kitu cha kutazama. Si kuangaliana mmoja na mwenzake; angalia kule kwa kile alichu Yeye, kile, ambacho, Yeye aliinuliwa juu kwenye kiti Chake cha enzi.

¹¹⁹ Angalia Maserafi wa Mbinguni wamefunika nyuso Zao. Sasa, Maserafi ndio wateketezaji wa dhabihu, ambacho ni mojawapo ya vyeo vikubwa sana vya Malaika. Ndio wa pili baada ya Makerubi. Pale palikuwa ni Malaika, na kisha Maserafi, na halafu Makerubi. Na Maserafi hasa ndio wateketezaji dhabihu, wakiandaa njia ya kukaribia kwa mwenye dhambi, kiwango cha juu kweli cha utakatifu katika hekalu la Mungu.

¹²⁰ Ndipo akaona, wakati alipokuwa chini kwenye sakafu hekaluni, akiomba, “Bwana, mimi ni mtu mwenye midomo michafu, na ninaishi miongoni mwa watu wachafu.” Na alikuwa akifanya maungamo yake.

¹²¹ Basi alipofanya hivyo, aliangalia juu akawaona hawa Maserafi. Walikuwa na mabawa mawili juu ya nyuso Zao, na mabawa mawili juu ya miguu Yao, na walikuwa wakiruka kwa mabawa mawili, wakiitana, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu ni Bwana Mungu Mwenyezi! Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu,

yote ya Mungu ni mtakatifu! Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu ni Bwana Mungu Mwenyezi!”

122 Hebu tuangalie ono aliloota nabii, na kulichambua. Mabawa mawili yalifunika nyuso Zao. Wazia hilo, hata Malaika watakatifu iliwabidi kuficha nyuso Zao zisizo na dhambi, kusimama katika Uwepo wa Mungu. Walipewa mabawa kuficha uso Wao, katika Uwepo wa Mungu mtakatifu! Mimi na wewe tutasimamaje Kule, kama Maserafi iliwabidi kutumia mabawa, njia ya Mungu iliyotolewa kuficha Uso Wao, kusimama katika Uwepo Wake, kuimba, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu ni Bwana Mungu Mwenyezi”? Kicho katika Uwepo wake!

123 Sasa hatuna uchaji wowote kwa Mungu. Kila mtu anafikiria tu kuwa yuko salama sana, mpaka wao—wao hawaninii—wao hawamchi Mungu jinsi wanavyopaswa kumcha. Kwa nini? Kwa nini wanafanya hivyo? Kwa sababu hawautambui Uwepo Wake. Hiyo ndiyo sababu watu wanafanya hivyo. Wao, wao hawautambui. Hawawezi, hawawezi kufahamu kuwa wako katika Uwepo wa Mungu. Akili zao zinapotoshwa sana na kutwaliwa na mambo ya ulimwenguni, mpaka hata hawauzingatii hata kidogo. Wanaenda kanisani, hakika. Lakini kutambua ya kwamba uko katika Uwepo wa Mungu! Sio tu kanisani; popote ulipo, uko katika Uwepo wa Mungu.

124 Laiti wanalifanya kama Daudi alivyosema, “Daima namweka Bwana mbele ya uso wangu, hivyo basi sitatikisika.” Mradi tu Bwana alikuwa mbele zake, asingeweza kutikisika.

125 Basi hawa wateketeza dhabihu wa Kimbinguni wakiwa na mabawa nyusoni Mwao, huku wakiitana, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu,” kusimama katika Uwepo wa Mungu, ni nini kitakachotendeka kwa watu wenye dhambi ambao hawatamcha Mungu?

126 Mnasema, “Vema, Ndugu Branham, ndio kwanza useme walipewa mabawa mawili.”

127 Nawe umepewa kitu, pia, Damu ya Yesu Kristo. Hicho ndicho kifuniko chako. Hiyo, wewe husimami kama Serafi, husimami kama Kerubi, husimami kama Malaika. Bali, unasimama kama mwana au binti wa Mungu aliyekombolewa, na Damu hii. Haikupasi kuwa na mabawa haya waliyokuwa nayo. Hayo ni vifuniko maalumu kwa ajili Yao katika Uwepo huo. Bali wewe unayo Damu ya Yesu Kristo kama kifuniko, kusimama Huko. Sasa vipi... Sasa, wewe, iwapo una Damu hiyo, basi unamheshimu Mungu, unampenda Mungu, unamtii Mungu; na Mungu ni Neno.

128 Sasa angalia, pili, kwa mabawa mawili walifunika miguu Yao. Hiyo ilimaanisha nini? Unyenyekevu mbele za Mungu, katika Uwepo Wake.

¹²⁹ Kama vile Musa kwenye kichaka kilichowaka moto, alivua viatu vyake, alipomsikia akisema, “MIMI NIKO AMBAYE NIKO.”

Paulo, njiani akienda huko chini Dameski, a—alianguka kifudufudi.

¹³⁰ Yohana, alipoona Ro—Roho wa Mungu juu ya Yesu, alisema, “Nina haja kubatizwa na Wewe, na mbona Wewe waja kwangu?”

¹³¹ Huu hapa mfano mzuri. Daima tambua ulivyo mdogo, si ulivyo mkubwa.

¹³² Leo hii, sisi—sisi Wamarekani, sana, kwamba tunajaribu kuwazia kwamba sisi ni mkubwa fulani, “Sisi ni washiriki wa kitu fulani kikubwa, shirika fulani kubwa, kitu fulani kikubwa mashuhuri kilicho na . . .” Loo, kikubwa mashuhuri, kikubwa, kikubwa ndiyo yote tuonayo.

¹³³ Na kwamba wakati . . . Wakati mmoja, katika Biblia, tunao mfano wa hiyo. Kulikuwako na na—nabii aliyeingia kwenye pango na . . . Eliya. Naye Mungu alikuwa akijaribu kuvuta usikivu wake, atoke nje. Ndipo kukaja moto, na moshi, na—na pepo kali kupitia milima, na ngurumo, na matetemeko ya ardhi, na kutikisika, na kila kitu kingine. Nabii hata hokusogea. Mungu hata hakuwa katika hayo. Bali wakati ile Sauti ndogo, tulivu iliponena, alifunika uso wake na akajitokeza. Wakati ile Sauti ndogo, tulivu ya Neno la Mungu inaponena, si ulaghai, si madhehebu yetu makubwa, si kitu chetu fulani kikubwa, bali ile Sauti ndogo, tulivu, ya Neno, inayopuuzwa. Hiyo yafaa kumwita mtu kwenye toba. Mungu katika Neno Lake!

¹³⁴ Hata hivyo, Yeye alifunika miguu Yake; na kutambua ninii Yake . . . udogo wetu mbele za Mungu.

¹³⁵ Tatu, Yeye angeweza kuruka kwa hayo mengine mawili.

¹³⁶ Sasa kumbukeni, mawili, alifunika uso Wake, katika Uwepo wa Mungu, na kuwa na kicho. Pili, mabawa mawili juu ya miguu Yake yalimaanisha unyenyekevu, mbele za Mungu. Na jozi ya tatu ya mabawa, sasa, alijitia Mwenyewe katika kutenda. Angeweza kuruka kwa hayo mabawa mawili, unaona. Mawili juu ya uso Wake, mawili juu ya miguu Yake, na akiruka kwa mawili, sasa hiyo ilikuwa ni nini? Uchaji, unyenyekevu, na katika matendo.

¹³⁷ Mungu alimwonyesha nabii jinsi mtumishi Wake aliyeandaliwa hana budi kuwa; mwenye kicho, mnyenyekevu, na katika matendo. Sasa aliona kitu fulani tofauti na Uzia alichotoa. Alikuwa akimwonyesha nabii kile kimpasacho kuwa, si kama Uzia, bali kuwa kama hawa Makerubi wa Mbinguni. Na iwapo unataka kumtazama mfalme, mfalme wa duniani . . . Mtazame wa Mbinguni, ameinuliwa juu ya Mbingu zote, na vazi Lake likajaza Mbingu.

¹³⁸ Hapo tunaona kwamba alikuwa akimpa kitu cha kuangalia, kumshawishi tofauti na kile alichokuwa akiangalia, akiwazia, “Mtu aliyemtumikia Mungu na kusitawi, na kila kitu, alikuwa sawa.” Bali Isaya akaweka nia ya—yake juu ya mwanadamu.

¹³⁹ Naye mwanadamu ameshindwa, kwanza kabisa. Sijali yeye ni nani. “Amezaliwa katika dhambi, akaumbwa katika uovu, akaja ulimwengu akisema uongo,” kwa hiyo ameshindwa kabisa. Sijali kama yeye ni askofu, papa, mzee wa jimbo, au chochote kile awezacho kuwa. Yeye ameshindwa, kwanza kabisa, wala usimwangelie mmoja. Sijali, “Ingawa anahamisha milima kwa imani, na ingawa anatoa mali yake yote kulisha maskini.” Hata hivyo, mwangelie Yesu Kristo. Yeye Ndiye. Mtazame Yeye, si mtu fulani.

¹⁴⁰ Tunaona sasa kwamba alikuwa akionyesha hapa kile mtumishi wa Mungu hana budi kuwa, jinsi ni lazima awe mnyenyekevu na mwenye kicho na katika matendo.

¹⁴¹ Ingia katika matendo! Wengi wetu wanaweza kuwa wanyenyekevu, wengi wetu wanaweza kuwa na kicho, bali ni vigumu kuwaingiza katika matendo.

¹⁴² Lakini sasa tunaona kwamba Mungu alikuwa akionyesha jinsi alivyokuwa akimwandaa mtumishi Wake, kile kimpasacho kuwa. Hao Makerubi walikuwa, ama—ama Maserafi, walikuwa ni watumishi wa Mungu.

¹⁴³ Angalia, kama vile yule mwanamke kisimani, wakati alipokuwa akitazamia Andiko kutimia. Tulilozungumzia, mara mbili au tatu juma hili. Wakati, alikuwa akitazamia hilo kutimia. M—msichana huyo, kadiri tujuavyo, hakuenda kanisani. Yeye labda... Walikuwa mbali sana na Neno, na mambo kama hayo, wao... na kuita kanuni zao za imani na kadhalika. Kama Yesu alivyosema, “Mmechukua mapokeo yenu, na kulitangua Ne—Neno la Mungu.”

¹⁴⁴ Ni karibu jambo lilo hilo leo hii. Kanuni za imani tunazofundishwa, na kadhalika, zimelitangua Neno la Mungu. Neno haliwezi kutokea. Na mambo yanayosemwa, kweli; wamejazwa kasumba ya kitu kingine sana, hawawezi kuona Hilo.

¹⁴⁵ Kumbukeni, Sauti hiyo itarudia mara kwa mara si nyinyi pekee hapa. Kanda hii inaenda kote ulimwenguni. Mimi kwa hakika si kwamba ninawazungumzieni nyote hapa. Bali kama kuna mtu hapa anayehitaji hilo, vema, hilo, ni kwa ajili yako basi. Mnaona? Bali, kumbukeni kwamba Sauti hiyo itakurudia mradi tu ungali hai. Katika siku ya kufa kwako, itakurudia. Itii Hiyo! Rudi!

¹⁴⁶ Mapokeo yetu yamelichukua Neno la Mungu na kulitangua. Neno la Mungu likidhihirishwa, nao watu wanasimama karibu na kusema, “Vema, nadhani hilo ni la kupendeza mno.” Mnaona? Jamani, loo, jamani! Lafaa kuupasha moto moyo wako. Lafaa

kufanya jambo, bali halifanyi. Halifanyi hilo. Tunamwona Mungu...

¹⁴⁷ Wakati mwanamke huyu...Hao makuhani na kadhalika, labda hakuenda kanisani maana hakuona sababu yoyote ya kuenda, ya kitu kama hicho. Lakini alikuwa amesoma Maandiko. Kwa kuwa tazama, alijua, upesi, wakati Yeye alipomwambia kilichokuwa tatizo lake, mbona, alisema, "Mbona, tunajua kwamba Wewe huna budi kuwa ni nabii. Hatujakuwa na mmoja kwa mamia ya miaka. Lakini Wewe hapana shaka ni nabii, tunajua." Sasa, mnaona, maoni yangu, yeye aliwazia...

¹⁴⁸ Iwapo utayasoma maelezo ya pambazoni hapo, kisha uyasome katika Maandiko yako, yanarudi kwa "yule Nabii," ambaye alikuwa ni Kristo.

¹⁴⁹ Kasema, "Tunajua sisi...Hapana shaka Wewe ni nabii. Tunajua kwamba Masihi, atakapokuja, hili ndilo atakalofanya. Atatambulishwa na hili."

Ndipo Yesu akasema, "Mimi Ndiye ninayezungumza nawe."

¹⁵⁰ Akaingia katika matendo. Asingeweza kuvumilia zaidi. Kitu kile hasa walichokuwa wakitazamia, kilikuwa duniani wakati huo, naye aliona Hicho. Haijalishi jinsi alivyokuwa katika hali mbaya, kahaba, ama mwanamke wa jinsi hiyo, asingeweza... Watu mtaani hata wasingeweza kumsikiliza. Wasingemsikiliza leo hii. Lakini kumkomesha, ungewezaje kumkomesha? Ilikuwa ni kama nyumba inayoungua moto, kwenye upepo mkali. Usingeweza kuuzima. Moyo wake ukaanza kuwaka moto.

¹⁵¹ Akasema, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini kuwa Huyu ndiye Masihi?" Na ikakolea, pia. Ambapo, haikumlazimu Yesu kufanya hivyo mara nyingine tena. Watu walimwamini kwa sababu... walimwamini Yesu kwa sababu ya ushuhuda wa mwanamke huyu. Unaona? Ulifanya nini? Alikuwa mnyenyekevu, mwenye kicho, na katika matendo. Aliingia katika matendo alipoona jambo hilo likitukia.

¹⁵² Ishara Zake zafaa kushawishi, leo hii. Ishara zilizoahidiwa za siku hizi, Neno lililoahidiwa lililowekwa kwa ajili ya siku hii, kumwona Mungu akitimiza yale aliyosema angefanya, hilo lafaa kutufanyia jambo fulani. Lakini halifanyi.

¹⁵³ Kama tu lilivyowafanyia Wayahudi. Walikuwa wa kidini sana hata ha—hawakufikiria walihitaji Hilo. Wao, wao walidhanja walikuwa na kila kitu.

¹⁵⁴ Na hivyo ndivyo ilivyo na ulimwengu leo hii. Una chakula kingi, mavazi mengi, makanisa ya kupendeza, sehemu kubwa kubwa, wahudumu wazuri wenye elimu, na hivyo basi hawahitaji chochote kingine. "Bali hamjui," Maandiko yalisema, "ninyi ni uchi, wenye mashaka, vipofu, wala hamjui." "Hamjui," wala huwezi kuwaambia vingine. Wanaendelea kutembea moja

kwa moja katika njia hiyo, na kushindwa kuliacha Neno la Mungu kuwashawishi kuamini kuwa Yesu Kristo amefufuka katika wafu, na yu hai leo, yeye yule jana, leo, na hata milele, akijionyesha Mwenyewe hai. Kwa urahisi wao wamekufa tu. Kila mahali, kila uendako, inaonekana kuwa ni jambo lile lile. Ilibidi iwe hivyo, hata hivyo, mwajua. Hana budi kutolewa nje ya kanisa. Hakuna njia kabisa ya hilo kukosa kuwa hivyo. Mungu alisema itakuwa hivi. Lakini ikiwa—ikiwa . . .

155 Acha hiyo ikutikise, ikutikise vizuri. Haijalishi uko katika nchi gani, popote ulipo, uwe ni nani, acha ikuamshe.

156 Saa huja na kuenda. Kitu cha kwanza unajua, utakuwa unasema, “Vema, ni—nilidhani kulipaswa kuwa na hili likitukia kabla ya Unyakuo.”

157 Huenda kukawa na Sauti itakayorudi kama ilivyofanya wakati mmoja, “Imetendeka tayari wala hamkujua.”

158 Utafungwa kabisa kwenye kanisa mahali fulani, ukisema, “Mimi ni salama tu niwezavyo kuwa,” na, muda si muda wajua, Unyakuo utakuwa umekwisha. Utakuwa ni kuondoka upesi, kisiri, hakuna mtu anayejua chochote kuuhusu. Ulimwengu utaendelea tu moja kwa moja.

159 Kama Nuhu alivyoingia kwenye safina. Mnakumbuka, baada ya Nuhu kuingia kwenye safina, alikaa humo siku saba baada ya Mungu kufunga mlango. Mungu alifunga mlango, ndipo Nuhu akakaa ndani ya safina siku saba kabla ya chochote kutokea.

160 Nao mlango wa rehema utafungwa machoni pako, na huenda umefungwa tayari. Basi liwazie tu, watu wataendelea moja kwa moja kuhubiri, watu wakidhani wanaokoka, wakiweka majina yao kwenye vitabu, kujiunga na kanisa, wakipaza sauti, wakirukaruka.

161 Mbona, nimewaona Waislamu wakipaza sauti. Nimesikia . . . watu hunywa damu kutoka kwa fuvu la kichwa cha binadamu, na kunena katika lugha, na kufanya mambo hayo yote. Hiyo si ishara kuwa umeokoka. Loo, la.

162 “Wakiwa na mfano wa utauwa.” Ni nini “Nguvu zake” wanazozungumzia?

163 Mnaona, mambo hayo yangeweza kutukia, na utakuwa ni wakati uliopita wala hamtajua. Huwezi kubahatisha namna hiyo. Msifanye hivyo, enyi marafiki. Ingieni wakati mnapoweza. Msishawishi na jengo fulani kubwa mashuhuri, dhehebu fulani kubwa mashuhuri, msomi fulani mashuhuri mwenye akili nyingi. Acha Neno la Mungu likushawishi. Hilo hasa ndilo lililowasababisha wale wanafunzi. Walipoona Neno hilo limedhihirishwa, hilo liliwashawishi, “Tuna hakika!”

164 Lafaa kunukuliwa tena. Yesu, pamoja na umati wa maelfu wakimfuata, alisema, “Hao ni wengi kupita kiasi. Angalia,

angalia, kitu cha ajabu hapa, wapo wachache wameitwa... Naam, wengi wameitwa, wachache wamechaguliwa.”

¹⁶⁵ Kwa hiyo basi akaona makusanyiko makubwa, akasema, “Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, kunywa Damu Yake, hamna Uzima ndani yenu.” Hakulielezea.

¹⁶⁶ Nashangaa iwapo angesema hivyo huku Beaumont, leo, haijalishi jinsi alivyo maarufu, unafikiri madaktari, na watu waliostaarabika, na wanasayansi, wangesema nini? “Huyo mtu ni mumiani. Vema, Yeye anawataka muinywe Damu Yake? Vema, ni wa aina gani... Mnaingia kichaa.”

¹⁶⁷ Yesu hakulieleza kamwe. Alitaka kuwaondolea wanyonyaji mbali Naye. Hiyo ni kweli. Ndipo wote wakasimama na kuondoka.

¹⁶⁸ Ndipo akageuka na kuwaangalia wale mitume ambao hawakukusudiwa Uzima, bali Yeye alikuwa amewachagua. Hawakukusudiwa. Akasema, “Mtasea nini mtakapomwona Mwana wa Adamu akipaa Mbinguni alikotoka?” Loo, hicho kilikuwa ni kikata pumzi. Ni nini Yeye... .

¹⁶⁹ Hao—hao wahudumu wakasema, “Ati kupaa juu kuingia Mbinguni? Vema, Mtu huyu alizaliwa papa hapa Galilaya. Alizaliwa Nazareti. Tunamjua mama Yake, ndugu Za—Zake. Tunajua kitanda alimopembezewa. Tuliziona nguo Zake za kitoto. Tulizungumza na mama Yake. Halafu kusema Mtu huyu alikuja, ati kurudi mahali alikotoka? Alitoka Nazareti. Ni nini anasema, ‘ati Mbinguni?’”

¹⁷⁰ Kamwe hakulielezea. Wanyonyaji wengi kupita kiasi bado. “Wakaamka, wala hawakutembea na Yeye tena.” Hiyo ndiyo Biblia iliyosema.

¹⁷¹ Ndipo akageuka na kusema, “Mimi... .Ninyi nyote mwataka kwenda, pia?” kwa hao kumi na wawili.

¹⁷² Kumbukeni, wasingeweza kulieleza, bali walilijua. Walijua Yeye alikuwa, kwa hiyo wakamwambia. Alikuwa amewashawishi kwa ishara Zake zilizothibitishwa kutoka kwa Mungu. Angalia.

Alisema, “Mnataka kuenda, pia?” kwa wale kumi na wawili.

¹⁷³ Petro akasema, “Bwana, twende kwa nani? Kwa kuwa tuna hakika... .” Sasa, hilo, angalia, chunguza hilo. Ni kitu gani? “Tunajua kile Neno linasema kwa ajili ya siku hii. Tunajua kile Masihi anapaswa kufanya ajapo leo hii. Tumeliona jambo hili likitimizwa na Mungu.”

¹⁷⁴ Alilisema baadaye, kwenye Pentekoste. Yeye alisema, “Yesu mnazareti, Mtu aliyethibitishwa na Mungu miongoni mwenu, kwa mambo anayopaswa kutenda. Nanyi mmemchukua Mfalme wa Uzima na kumsulubisha, na—na Mungu akamfufua, ambalo nyinyi ni mashahidi wa hilo.”

Tazama hapa, unaona, alisema, “Twende wapi?”

¹⁷⁵ Yesu akasema, “Niliwachagua kumi na wawili, na mmoja wenu ni shetani.”

¹⁷⁶ Na wapo kumi na mmoja tu wamesimama hapo, kutoka kwa maefu mara maelfu. Kumi na mmoja wamesimama hapo. Loo, jamani! Wameshawishika! Hakika.

¹⁷⁷ Maskini mwanamke huyu, wakati aliposhawishika, aliingia katika matendo. Ilimbidi kufanya jambo kulihusu. Ilimbidi kumwambia mtu mwingine.

¹⁷⁸ Na kila nafsi halisi inayomgusa Kristo, huna budi kumwambia mtu mwingine kuhusu Hilo.

¹⁷⁹ Petro, alipomwamini kulingana na Neno Lake, usiku ule baharini, akamwona huko nje, alikuwa . . . ama siku ile, ilikuwa. Walikuwa wamevua usiku kucha, wala hawakushika chochote, wamevuta juya huku na huku. Huo ni wakati wa kuvunjika moyo, yeyote akiwa ni mvua samaki. Wakavuta juya usiku kucha, naye alikuwa ni mvuvi, pia. Baba yake alikuwa ni mvua samaki. Alishakuwa kwenye ziwa hilo maisha yake yote, na wazazi wake na babu zake walitoka kwenye ziwa hilo. Naye alijua wakati mwezi ulikuwa sawa, na jinsi upepo ulikuwa ukivuma, na dalili zote. Naye alivua samaki ili kupata riziki. Kwa hiyo alikuwa amevua usiku kucha, wala hakupata kitu.

¹⁸⁰ Ndipo wakagundua, kesho yake, kwamba—kwamba walisema Nabii huyu alikuwa anaenda kuhubiri, chini ufukoni. Nami nawazia, kutoka kwenye vibanda vyao wakaja maskini wanawake, na kadhalika, wakija kumsikia. Umati ukawa mkubwa mno, kando ya ufuko, ilimbidi kuazima merikebu hii, na merikebu ya Petro. Kutoka na kuosha nyavu zao, huku hawana hata samaki mmoja, kisha wakazitupa huko juu; walivunjika mioyo.

¹⁸¹ Na wakati mwingine kwenye majira hayo ya kuvunjika moyo, kama utaangalia, huo ndio wakati Yeye huja karibu. Ila usiwe kipofu kutosha kuikosa. Mnaona? Unapoona kila kitu kikitendeka kama ilivyo ulimwenguni leo, usiogope. Unaona? Usiogope. Ku—kumbuka tu, Yeye aliahidi kukujia.

¹⁸² Basi sasa angalia anapokuja, Yeye alimwambia Petro, kasema, “Sasa tweka mpaka kilindini mkashushe nyavu zenu mvue samaki.”

¹⁸³ Petro akasema, “Labda. Sijawahi kuona hili likifanywa hapo awali. Si—sijui. Nimevua samaki, maisha yangu yote, hapa. Da—dalili, tumetoka tu kuvua, usiku kucha, kwenye maji yayo hayo. Na, hata hivyo, lakini hakuna kitu. Hatujashika kitu. Bali kwa Neno Lako, Bwana,” hilo hapo, “Nitashusha wavu. Neno Lako!”

¹⁸⁴ Huenda umepitia kila hospitali. Ndugu King, huenda wanasema kwamba unaenda kufa. Huenda wanasema, dada,

hili, lile, ama lingine. Sijali walilosema. “Kwa Neno Lako, Bwana, nitashusha wavu!”

¹⁸⁵ Alipoliona Neno hilo limethibitishwa, Yesu alipomwambia jambo fulani, aliliamini, na akaushusha wavu kwenye maji ambako hakukuwa na samaki. Lakini, kama Mungu alisema hivyo, Yeye aliweza kuweka samaki mle, sawa na alivyoweka maji angani.

¹⁸⁶ Anaweza kuweka uponyaji mwilini mwako, sijali kama hakuna kitu humo. Unamtumainia kuuinua katika siku za mwisho. “Kwa Neno Lako, Bwana, nitaushusha wavu.”

¹⁸⁷ Hiyo ilimshawishi sana huyo mvua samaki, hata akaacha samaki na kila kitu, na kumfuata Yesu. Ulikuwa ni ushawishi, alipomwamini katika Neno Lake. Basi Yeye alifanya nini?

“Vema,” akasema, “asante, Bwana, kwa pato zuri la samaki.”

Kasema, “Uache wavu wako. Tangu leo utavua watu.” Mtume huyo akaingia katika matendo!

¹⁸⁸ Hatimaye, kwenye mwisho wa safari, walipokuwa wanaenda kumsulubisha, kumwua, basi akatoroka mjini. Halafu njiani akitoka, kama historia inavyotwambia, alikuwa anakimbia kuokoa maisha yake, akiondoka mjini, ndipo akakutana na Yesu akirudi. Akasema, “Unaenda wapi, Simoni?” Au Simoni akamwambia, “Unaenda wapi, ewe Bwana?”

¹⁸⁹ Akasema, “Ninarudi ndani ya mji ili kusulibishwa tena.”

¹⁹⁰ Simoni akageuka na kurudi. Basi walipompata, kasema, msininii... Wakamweka msalabani. Kasema, “Msinitundike namna hiyo. Wekeni kichwa changu chini, na miguu yangu juu!”

¹⁹¹ Alikuwa ameshawishika alipomwona Yesu aliyefufuka kutoka kwa wafu; akashawishika kwa ajili ya kifo chake, alishawishika kwa ajili ya kitu chochote kile. Akaingia katika matendo. Mauti hayangeweza kukomesha hilo. Kusulubishwa hakungeweza kulikomesha. Alishawishiwa na Yesu.

¹⁹² Yule kipofu aliyeponywa. Walimwambia anyamaze, lakini yeye alisambaza umaarufu Wake kila mahali. Watu wake walisema, sasa, makuhani walisema, “Sasa mtu yeyote akienda na kuhudhuria uamsho huo, watakuja tu wachukue makaratasi yao ya kanisa, hivyo tu.” Na baba na mama yake waliogopeshwa na hilo. Mnaona? Kwa hiyo wakasema... .

Walikuja, wakasema, “Mvulana huyu alipataje kuona?”

Kasema, “Yeye—yeye ni mtu mzima; mwulizeni.” Waliogopa.

Lakini yule aliyekuwa ameponywa alishawishika. Amina.

¹⁹³ Akasema, “Mtu huyu ni mwenye dhambi. Mpe Mungu sifa! Hatujui anakotoka Mtu huyu. Yeye hana—Yeye hana stakabadhi zozote. Hatushirikiani na Yeye. Hatuna uhusiano wowote Naye.

Hatujui anakotoka. Tunajua Yeye ni mwenye dhambi na—na anatoka kwa ibilisi.”

¹⁹⁴ Mtu huyu alikuwa na jibu zuri kwa hao. Alisema, “Sasa hili kweli ni jambo la kushangaza.” Kasema, “Sasa, ninyi mnapaswa kuwa ndio viongozi nchini. Naye Mtu huyo amenifumbua macho, na hata hivyo hamjui mahali anakotoka.” Akasema, “Sasa, kama Yeye ni mwenye dhambi, au sivyo, sijui hayo. Bali jambo hili moja ninajua, kuwa mimi nilikuwa kipofu, sasa naweza kuona.”

¹⁹⁵ Alikuwa ameshawishika. Hakujali kusimama mbele za makuhani au chochote kile. Alikuwa ameshawishika. Wazazi wake, hata mwujiza juu ya mwana wao wenyewe haukuwashawishi, bali ulimshawishi yeye.

¹⁹⁶ Watu kwenye Pentekoste, kama nilivyosema jana usiku, pamoja na hati yao ya Uzima wa Milele, wakati walipoenda kuchukua ninii yao...faida kwa Hiyo. Angalia waliposhawishika. Walikuwa watakatifu, wakawa na kicho mbele za Mungu. Walikuwa wamezifunika nyuso zao kutokana na mambo ya ulimwengu, na miguu yao katika unyenyekevu. Basi walipohisi Nguvu za Mungu zikija, kama ilivyoahidiwa na Yoeli, kama ilivyoahidiwa na manabii, kama ilivyoahidiwa na Yesu! “Ngojeni huko juu katika mji wa Yerusalemu mpaka mtakapojazwa na Nguvu kutoka Juu.” Punde tu Mungu huyo, katika Utu wa Roho Mtakatifu, aliposhuka juu yao, walishawishika. Hawakujali ni watu wangapi waliowacheka. Waliingia mitaani, wakiyumbayumba kama walevi. Walishawishika na Roho Mtakatifu. Waweza kushawishika, pia. Walisimama moja kwa moja . . .

¹⁹⁷ Mwangalie. Hakuzunguka huku na huku na kukariri namna fulani ya kanuni ya imani. Alirudi moja kwa moja kwenye Neno, na akasema, “Enyi watu wa Yerusalemu, ninyi mkaao Uyahudi, na ijulikane kwenu, na myasikie maneno yangu. Hawa hawajalewa kama mnavyodhani, kwa maana ni saa tatu ya mchana. Lakini hili ni Lile lililonenwa na nabii Yoeli, ‘Na itakuwa katika siku za mwisho,’ asema Mungu, ‘Nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili.’” Walishawishika na Neno, kwa Neno. Linapaswa kutufanya vivyo hivyo.

¹⁹⁸ Wakaingia katika matendo, naam, wakati ahadi Yake ilipotimizwa. Wakati, walipoona kwamba Yesu aliwaahidi kwamba Yeye angeituma ahadi ya Baba juu yao, Luka 24:49, “Tazameni, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba Yangu; lakini ngojeni.” Kungoja hakumaanishi omba, kunamaanisha tu kusubiri. Ngoja inamaanisha “subiri.” “Ngojeni huko juu kwenye mji wa Yerusalemu hata mvikwe Uwezo utokao Juu.” Basi ushawishi huu wa Roho Mtakatifu ulipowaangukia, Huyo aliwajaza. Wakaliona Neno, ambalo Yesu aliahidi, limetimia.

¹⁹⁹ Sasa, sijui kama itahitaji ushawishi uo huo juu yetu alasiri ya leo? Tukiona kile Yeye alichohidi kufanya katika siku za

mwisho, kikitimia, Hicho kingetupa ushawishi wa namna gani? Kitu gani? Yote ambayo tumeona yakifanywa katika siku hizi za mwisho yanapaswa kutuingiza katika matendo. Kwa kweli yanapaswa kutuingiza, pamoja na uchaji na unyenyekevu.

²⁰⁰ Bila tashwishi yoyote, dai lililotolewa yapata miaka thelathini iliyopita, kuhusu Nguzo ya Moto, ambayo kamera ziliipiga picha. Kamera yenu ya Texas iliipiga picha si muda mrefu uliopita. Utafiti wa kisayansi, uliipitisha kwenye kila aina ya utafiti walioweza kupata, kwa FBI. Pia . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . Ikapigwa Texas, kwa ajili ya Mtexas. Ukiiona ishara, haiwezi kukanushwa. Ni kweli. Lakini je! mtaimini Sauti inayoifuata hiyo ishara? Ishara imethibitishwa kisayansi. Sasa, siku moja wakati Yesu atakaporudi na kunyakua watu, wote jinsi walivyo, itajulikana, pia.

²⁰¹ Tazama, Nguzo ya Moto yafaa ituingize katika matendo, jinsi Nguzo ya Moto inavyohibitisha ahadi Yake ya siku za mwisho. Yesu alisema, “Nalitoka kwa Mungu, tena narudi kwa Mungu,” na kile angefanya katika siku za mwisho. Naye Huyu hapa, kisayansi na kiroho pia, katika Neno akithibitisha, kwamba alitoka kwa Mungu na angali anadumu yeye yule. Angali ni Mungu, kwa ajili ya ahadi katika siku za mwisho. Hiyo yafaa kutuingiza katika matendo.

²⁰² Ishara za Kuja zimewadia. Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa huko Sodoma, kabla tu ya ulimwengu kuteketezwa, ulimwengu wa Mataifa,” hii ingejirudia. Inafaa kutushawishi na kutuingiza katika matendo, pia. Tunapoliona Neno likitimia, aliloahidi, linafaa kutuingiza katika matendo.

²⁰³ Sisi, kama vile nabii, tumeona matokeo ya madhehebu yaliyojikweza, yakipoteza mahali pao. Nataka hiyo izame hata kwenye kilindi, maana huenda nisizungumze nanyi tena. Lakini, wanaume na wanawake, hebu niseme jambo hili, na nizungumze nanyi kwa njia huru, alasiri ya leo, katika Jina la Yesu Kristo. Watu wenye mawazo ya busara, watu wasio na kiburi, walio mbali sana na Mungu kwa mapokeo; kwamba, wameliona kanisa la Pentekoste, mmeona la Kibaptisti, Methodisti, na Presbiteri, mmeliona kanisa Katoliki, likipoteza mahali pake katika Mungu, wakipoteza msimamo wao katika Neno, walipokubali kanuni za imani.

²⁰⁴ Ni—nilihojiwa na kasisi, si muda mrefu uliopita, naye akaniambia, akasema, “Mbona, mimi. . .” Akaniuliza kuhusu kitu fulani, na mambo haya. Akasema, “Vema, kanisa Katoliki lilikuwa likifanya hivyo.”

²⁰⁵ Nikasema, “Lini? Kanisa Katoliki halikufanywa dhehebu kwa miaka mia tatu baada ya kifo cha mtume wa mwisho.”

Akasema, akasema, “Unajaribu kuitetea kesi yako kwa Biblia.”

Nikasema, “Hiyo ndiyo Neno.”

Akasema, “Mungu yuko katika kanisa Lake.”

206 Nikasema, “Mungu yuko katika Neno Lake. Kila kitu kingine na kiwe uongo, na Lake liwe kweli.”

207 Naye akasema, “Vema, hicho ni Kitabu tu ambacho—ambacho Wakatoliki wa mwanzoni waliandika.”

208 Nikasema, “Basi mimi ni Mkatoliki wa mwanzoni. Ninaamini kile tu Hicho kimesema.” Sininii...nikasema ndipo...

Akasema, “Vema, unaona, sisi ni kanisa kubwa zaidi sasa.”

209 Nikasema, “Basi mmepotea wapi? Ni nini kilichotendeka? Ikiwa kanisa la mwanzoni lilitoa pepo, na kumthibitisha Yesu kuwa hai duniani, kwa ishara za kiroho na maajabu; na hapa mnao maelfu ya waombezi, wa kila namna ya wanawake waliokufa na wanaume waliokufa, na kila kitu, kufanya waombezi. Katika Biblia, papa wa kwanza alisema, kwamba, ‘Hakuna mpatanishi mwingine kati ya Mungu na mwanadamu ila Mwanadamu Yesu Kristo.’”

210 Kupoteza msimamo wako kwenye Neno, na kukubali kanuni za imani na majivuno kwa ushauri wa mwanadamu, tumewaona wakipoteza msimamo wao na Roho Mtakatifu mkuu. Tumewaona Wapentekoste wakifanya jambo lile lile. Nanyi mnaliona. Wanapojiundia dhehebu, wanakufa. Hamna njia ya kurudi; haijawahi kuwepo, na kamwe haitakuwepo. Mungu anachukia kitu hicho. Kwa kweli ni dhambi. Kasema, katika siku za mwisho Yeye angesema, “Ondokeni kati yao, enyi watu Wangu, ili msiguse vitu vyao vichafu; Nami nitawapokea.”

211 Kama vile Uzia, alijaribu kufanya nini? Alijaribu kupachukua mahali pa ofisi iliyopakwa mafuta, ofisi ya Mungu iliyopakwa mafuta. Uzia alijaribu kunyakua mamlaka hayo, kwa kuwa alikuwa ni mtu mashuhuri.

212 Tumeyaona haya madhehebu ya kujibunia yakisonga kabisa na kuondolea mbali chochote kilicho Mungu, huku yakijaribu kuchukua ofisi ya Kanisa, Kanisa lililopakwa mafuta. Basi kwa kanuni za imani, tumeona ya kwamba yamekufa kwa kutokuamini, wala hayatafufuka tena. Yatakufa katika kambi ya wenye ukoma pamoja na hao wengine.

213 Mnaona hapo? Watu, watu wenye busara, watu wanaoamini Maandiko wanaona hilo. Iwapo umezaliwa na Mungu, unaliona. Mungu akilitambulisha jambo hilo dhahiri sana, kukushawishi. Kama ambavyo tumehubiri wiki nzima, na kadhalika, kile linachopaswa kufanya, kuvuta usikivu. Linakushawishi, kuona mahali wamefikia na kile kilichotokea, kila mmoja wao.

214 Wakiunda dhehebu lingine, litafanya jambo lile lile. Bali hakutakuwepo na mengine zaidi. La. Hayo, yamekwisha sasa. Kumechelewa sana sasa.

215 Wakipoteza msimamo wao, kwa kukubali kanuni za imani na mafundisho ya kujibunia ya mwanadamu. Hao wanaogopa, kuja tu kusimama na Hiyo. Mnaona?

216 Kama vile Uzia akijaribu kunyakua mahali pa o—ofisi iliyopakwa mafuta, kwa kuwa alikuwa ni mtu mkubwa, jamaa mkubwa. Na miongoni mwa watu wa Mungu hapana watu wakubwa. Sisi sote ni watoto wa Mungu. Mungu humpa mmoja wetu kitu kimoja cha kufanya, na kitu kingine cha kufanya, hicho hakitufanyi bora kuliko yeyote mwingine. Humfanya tu Mungu kuhitaji mengi zaidi mkononi mwako, hivyo tu.

217 Sasa matokeo ya ono kama hilo, kisha tunafunga. Tutaanza kuwaombea wagonjwa, katika dakika chache. Sasa matokeo ya ono kama hilo. Hayo matokeo yalimfanyia nini nabii huyu? Sijui kuhusu mhubiri, sijui kuhusu mwinjilisti, ama mchungaji? Angalia kile ono la Hiki lilichofanya, na kile alichoon, kile kilitokea kwa Uzia aliyejiendeleza mwenyewe. Ndipo basi, ingawa alikuwa ni mtu mashuhuri ambaye Mungu alikuwa amemwinua, kitu kile kikuu, walikiona kimekufa. Hicho kilileta matokeo gani kwa nabii?

218 Hiki hapa kilichofanya. Kilimfanya kukiri mwenyewe kuwa ni mwenye dhambi kwa kujihusisha na kama hao. Alikiri, “Mimi ni mtu mwenye midomo michafu, pia nimekuwa nikiishi miongoni mwa watu wenye midomo michafu.” Ikimfanya ku- . . . nabii, si mhubiri. Nabii alikiri kwamba alikuwa ni mtu mwenye dhambi, kwa kuwa alikuwa akijihusisha na walio hivyo.

219 Ndipo nini? Alipokiri dhambi zake, ndipo kukaja kusafishwa. Loo, huwezi kuwa safi kutokana na dhambi zako mpaka kwanza ukiri kwamba ni dhambi, mpaka utambue kwamba ni dhambi. Ndipo kukaja kusafishwa, punde tu aliposema, “Ole wangu, kwa kuwa macho yangu yameona thibitisho la Mungu mkuu. Malaika, Wateketezaji, Watoa dhahihu wako hapa, na vizingiti vinatikisika kwa Sauti Yao, nao Hawa hapa katika ono hili, wakiruka huku na huku.” Alikuwa ameona kitu halisi. Ono lilikuwa limeshuka. Akasema, “Mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa miongoni mwa watu wachafu.” Kasema, akalilia rehema na kujiita mwenyewe mwenye dhambi.

220 Ndipo kukatokea nini? Mmoja wa Makerubi alienda kwenye madhabahu, akatwaa makoleo na kuchukua kaa la moto, akaliweka mkononi Mwake. Si kulibeba kwa koleo sasa; akalitwaa hilo kaa, akaliweka mkononi Mwake, kisha akaja na kuliweka juu ya midomo ya nabii, na kusema, “Uovu wako . . .”

221 Uovu, uovu ni kitu gani? Uovu ni jambo unalojua kuwa ni makosa, na ungali unalishikilia. Wakati unajua kwamba kanuni zako za imani si sahihi, na ungali unazishikilia, huo ni uovu.

222 Bali alipokiri kwamba alikuwa makosani, kulikuwa na nguvu za kutakasa. Akatwaa kaa la Moto. Hivi mlitambua jinsi Mungu. . .

223 Tunaona jinsi Mungu alivyowaweka watumishi Wake katika utaratibu, na kile alichomwandaa nacho; jinsi alivyoweza, kuwa mnyenyekevu, mwenye kicho, na kujiweka katika matendo.

224 Angalia, wakati alipomtakasa huyo mtumishi, Yeye hakumtakasa kwa seminari. Hakumtakasa kwa lundo la vitabu. Tunaona hapa kwamba Mungu huwatakaswa watumishi Wake kwa Moto. Kaa la Moto lilimgusa nabii, likatakaswa midomo yake. Mungu huwatakaswa watumishi Wake kwa Moto Wake Mtakatifu. Si kwa vitabu, si kwa elimu, theolojia; bali alimtakasa mtumishi Wake kwa Moto.

225 Ndipo mara alipokuwa amekiri na kutakaswa, basi agizo likafuata. Kwanza ilimbidi kukiri, halafu ilimbidi kutakaswa, na sasa ni agizo. Ilikuwa ni wakati huo ambapo Isaya aliyetakaswa alilia. . . Alipoisikia Sauti ya Mungu, kasema, “Ni nani atakayekwenda kwa ajili Yetu?”

226 Tazama nyuma katika historia, wakati unaposoma hili, ukienda nyumbani, kilichokuwa kimetokea kwa Israeli. Lilikuwa limefikia pale pale (mahali) tulipo. Walikuwa wameita. . . Kafara zao zote na kadhalika zilikuwa zimekuwa desturi kwao. Hakukuwapo na uaminifu wowote. Hawakuliheshimu Neno la Mungu. Hapo ndipo Mungu alipomwinua Isaya, kumwambia kuwa hizo kafara zilinuka katika pua Yake. Hakuzitaka. Zilikuwa ni makufuru Kwake, basi hakutaka uhusiano wowote nazo tena. Ndipo wakati. . . Huyu Isaya alitakaswa na tayari kwenda kuhubiri Injili wakati huo.

227 Ndipo Sauti ya Mungu ikasema, “Sasa kuna haja. Mambo haya hayana budi kusemwa.” Tena Sauti moja ikaambia nyingine, Malaika wakiruka, kasema, “Ni nani atakayekwenda kwa ajili Yetu?”

228 Ndipo Isaya, akiwa na moyo safi; ametakaswa, amekiri, akatakaswa na kuagizwa, lile ono; kasema, “Mimi hapa, Bwana, nitume mimi. Nitume mimi. Mimi hapa, nitume mimi.”

229 Mungu, watume Malaika Wako watakatifu tena leo. Mpate Isaya Wako mahali fulani, ombi langu. Mimi—mimi si. . . Ninasema tu haya maana ninajua Yeye yupo hapa.

Kaa la Moto lilipokuwa limemgusa nabii,
Likimfanya safi kabisa,
Wakati Sauti ya Mungu iliposema, “Ni nani
atakayekwenda kwa ajili Yetu?”
Ndipo akajibu, “Bwana, mimi hapa, nitume
mimi.”

230 Hakuogopa wakati huo akiwa na Neno. Alikuwa ni nabii; Neno lingeweza kumjia. Alikuwa. . . Kutokuamini kwake kwote

na mapokeo yalikuwa yametoweka. Angeweza kusimama mbele ya wakati huo wa kimapokeo, na kuwaambia, “Kafara zenu zinanuka katika pua ya Mungu. Na Mungu yule yule mnayedai kumtumikia, atawaangamiza.” Hilo ndilo alilosema. “Mungu yule mnayedai kuwa mnamtumikia, atawaangamiza,” na Yeye alifanya hivyo.

Wakasema, “Ishara!”

Akasema, “Nitawapa ishara kuu; bikira atachukua mimba.”

²³¹ Isaya aliandika sura sitini na sita katika Kitabu chake, na kuna Vitabu sitini na sita katika Biblia. Anaanza na mwanzo wa uumbaji, na kumalizia katika Utawala wa miaka elfu kama tu Biblia nzima ifanyavyo.

²³² Huyu nabii mashuhuri wa Mungu, aliyekuwa tayari kukiri kwamba mapokeo yao yote yalikuwa ni makosa; na kwenda huko chini na kutakaswa, na kwa hiyo Neno la Mungu lingeweza kumjia. Ndipo akasema, “Niko tayari kwenda, Bwana. Niko tayari. Nitasema kile Wewe umesema niseme. Nitasema kile Wewe umesema niseme.” Alikuwa tayari kwenda.

²³³ Mungu, walete Malaika tena, alasiri ya leo, Roho Mtakatifu na Moto, na utakase mioyo ya ndugu zangu, kila mahali. Jalia wawe ushawishi mkuu hata wengine wataona na kutamani kufuata, pia.

²³⁴ Na tuinamishe vichwa vyetu. Kwa utulivu:

Wakati kaa la Moto lilipokuwa limemgusa nabii,

Likimfanya safi kabisa,

Wakati Sauti ya Mungu iliposema, “Ni nani atakayekwenda kwa ajili Yetu?”

Ndipo akajibu, “Bwana, hapa, nitume mimi.”

Kwa utulivu sasa, sote pamoja.

Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,

Nena, nami nitakujibu upesi;

Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,

Nena, nami nitajibu, “Bwana, nitume mimi.”

Mamilioni sasa wanakufa katika dhambi na aibu;

Kisikilize kilio chao cha huzuni na uchungu;

Hima, ndugu, hima kuwaokoa;

Upesi jibu, “Bwana, mimi hapa.”

Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,

Nena, nami nitakujibu upesi;

Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,

Nena, nami nitajibu, “Bwana, nitume mimi.”

²³⁵ Hebu na tuuvumishe, kwa utulivu. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nena, Bwana Wangu—Mh.*] Hebu na tushuke kwenda hekaluni sasa.

Kisikilize kilio chao cha huzuni na uchungu;
(Loo, ndugu, njoo pamoja nami, hivi utakuja?)

Hima, ndugu, hima kuwaokoa; (Hawajui ni dhehebu gani, kujiunga nalo, au chochote)
Upesi jibu, “Bwana, mimi hapa.”

Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
(Kina Isaya, je, mpo hapa?)

...nami nitakujibu upesi,

Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,

Nena, nami nitajibu, “Bwana, nitume mimi.”

²³⁶ Nashangaa, huku vichwa vyenu vimeinamishwa na mioyo yenu imeinamishwa, Isaya, uko wapi? Hivi utainua mkono wako, na useme, “Bwana, mimi hapa, nitume mimi. Niko tayari?” Mungu awabariki. Sasa limaanishe kweli. Asilimia tisini ya wasikilizaji.

Nena, Bwana wangu,

Nena, nami nitajibu, “Bwana, nitume mimi.”

²³⁷ Angalieni, wahudumu, wewe uliyeinua mkono wako. Waangalie wanawake wetu, dada zetu, ni fedheha jinsi gani! Tsk, tsk, tsk, tsk, tsk, tsk! Waangalie wanaume wetu, wanawazia zaidi kuhusu dhehebu kuliko wanavyofanya kuhusu Neno la Mungu. Yesu Kristo akijithibitisha Mwenyewe miongoni mwao, na ni Maandiko hasa kwa udhahiri sana na kutambulishwa, na hata hivyo watashikilia moja kwa moja kwa hilo. Ndugu!

²³⁸ Mtu fulani aseme, “Vema, nisingekuwa na chochote. Mimi—mimi...kwamba wao...nisingekuwa na mahali popote pa kwenda.”

²³⁹ Ndugu, kama ilinibidi kula mkate mkavu na kunywa maji ya kawaida, ningekaa na Bwana wangu. Yeye ni uhai wangu. Yeye ni mkate wangu. Mnafikiri ninafanya hivi kuwa tofauti? Ninafanya hivi kwa sababu ninampenda, kwa sababu ni agizo langu. Kusimama bega kwa bega, pamoja Naye, pamoja na hilo Neno!

Loo, nena, nami nitajibu, “Bwana, nitume mimi.”

²⁴⁰ Baba wa Mbinguni, huku muziki ukiendelea kwa utamu, jalia kila mtu aliye katika Uwepo wa Kiungu, Bwana, aone kwamba huu ni wakati wa kuitwa. Ni—ni wakati wa utengano, wakati makapi na—na ngano zinafaa kutenganishwa. Ingawa nga—ngano ilikuwa imefunikwa kwenye kapi, bali sasa ni wakati wa kuitwa kutoka. Ni kutoka kwingine.

²⁴¹ Ninaomba, Mungu, kama vile Nuru kuu ya Mwana imeivisha punje kwa kila hatua ya Uhai wake, kuanzia wakati...Kama huko Canada sasa, wakati ngano ndiyo kwanza inakua, lile jua kali la Julai lingeiua sasa hivi, bali haina budi kukomaa

kulingana na vile maumbile yanavyoleta jua juu yake. Vivyo hivyo na jua kali la Mwana juu ya mafundisho ya Luther, Wesley na hao wengine, Hilo huichoma, bali ni la kuivisha ngano. Yafaa iwe imekomaa, Bwana, wakati Hilo likitokea.

²⁴² Lakini, kumbukeni, matawi yote yalipogolewa, nao mti wa Bibi-arusi ukatokea moja kwa moja katikati. “Nitarejesha, tena, miaka yote ambayo tunutu, madumadu,” mdudu yule yule, ila tu kwenye hatua mbali mbali, “amekula. Nitaurejesha,” ASEMA BWANA. Nawe utaurejesha, Bwana. Uliahidi hilo. Ninaomba kwamba utafanya hivyo katika kila moyo alasiri ya leo.

²⁴³ Hao ni Wako, Bwana. Ninawakabidhi Kwako sasa. Na huenda nisiwaone kamwe. Kama ningerudi, mwaka mmoja kuanzia leo, wapo wengi wanaoketi hapa, nikiwa hai, wao hawatakuwa. Hapana shaka, umati huu mkubwa, wakati mwingine nitakapokutana nao utakuwa kwenye Hukumu. Jalia waone, Bwana. Jalia wafungue macho yao, iwapo kuna ninii . . . na waone.

²⁴⁴ Hawa wote kwenye kanda, Bwana, ambao wameisikiliza Sauti ya wakati huu, lugha nyingi mbali mbali, hata itafsiriwe, jalia waelewe. Jalia wanaume na wanawake, katika vyumba vidogo, na huko nje katika maskini misitu huko Afrika, wakiwa na hizo mashine ndogo ndogo huku wana tyubu katika masikio yao, jalia wasikie, Bwana, wasikie. Jalia hilo. Mmishenari alikuwa sahihi katika kile alichosema, bali huu ni ushuhuda mkuu kuliko ule aliokuwa nao. Yuko tayari sasa. Tusikie, Baba. Tunayakabidhi yote Kwako, katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao, na kwa kuitwa kwa Bibi-arusi Wake. Amina.

²⁴⁵ Sasa, ndugu yangu, dada, tunaenda kuwaombea wagonjwa, kila mmoja wenu uliyeinua mkono wako. Si—siwezi kuutoa. Kama ningeweza kuwapa, ningefanya hivyo. Hakika, ni—ningeteremka moja kwa moja hapo na kusema, “Hapa, mnaitaka? Ni—nitakuwa nayo.” Si yangu kuwapa hiyo. Ni Mungu, na Mungu atakupa wewe ikiwa kuna njaa moyoni mwako.

²⁴⁶ Kabla hakujaweza kuwepo na wito kwa kilindi hapana budi kuwa na kilindi cha kuitikia wito huo. Kabla ya kuwepo na maumbile, hapana budi kuwepo na Muumba kuumba hayo maumbile.

²⁴⁷ Unajua kuna kitu fulani pale unachokiendea; hapana budi kuwepo na kitu fulani huko nje kuitikia wito huo. Hivi hutaipokea sasa? Usiiache ife. Tafadhali usifanye hivyo. Nisipowaona tena upande huu wa Hukumu, naomba niwaone Huko, mmeoshwa na tayari. Maombi yangu!

²⁴⁸ Sasa Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, Yule aliyeonekana duniani katika umbo la Mwanadamu, Mwana wa Mungu, Yesu Kristo; Yule aliyeteseka chini ya Pontio Pilato, akasulubishwa, akazikwa, akafufuka siku ya tatu; akapaa

Mbinguni, ambapo sasa ameketi kwenye mkono wa kuume wa Ukuu; akituma Roho aliyekuwa juu Yake kurudi, aitwaye Roho Mtakatifu, Mungu, juu ya, kuja juu ya wanadamu, kuwa na ushirika, kuendeleza huduma iliyoendelezwa katika ule mwili wenye utukufu wa Kristo. Unaotarajiwa... kuja kama piramidi inavyojengeka, namna *hiyo*, Jiwe la kichwa halikuwekwa juu yake. Kwa nini? Lilikataliwa.

²⁴⁹ Sasa, chini kabisa, kanisa daima limekuja katika uchache, limeinuka sasa mpaka nyakati zote za kanisa zimekwisha. Halina budi kuchongoka. Hilo jiwe halina budi kutoshea moja kwa moja. Huduma iliyokuwa ndani ya Yesu Kristo sharti iwe katika Kanisa Lake, kumfanya Kristo kulijia Kanisa, kuinua kila wakati, kumleta Yeye, kulitoa.

²⁵⁰ Kama tu vile ngano. Ngano haina budi kurudi moja kwa moja, inapoanza kukomaa, kutoka kwenye mbegu mahali ilipoozea, ikafa, na kuchipuka na kuendelea kukua kutoka kwenye unyasi kuwa kitu kingine. Huwezi kurudi kwenye unyasi. Usielekeze kurudi kwenye unyasi. Usielekeze kurudi kwenye *hii*. Usielekeze kurudi kwenye mganda. Njoo moja kwa moja mpaka ufikie kwenye ngano. Nayo ngano haina budi kuwa aina ile ile ya ngano iliyoingia ardhini, wakati imekomaa. Yesu amefufuka kutoka kwa wafu. Amekomaa sasa. Naye amekomaa katika Kanisa Lake, kupitia kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu; kupitia hawa warekebishaji katika siku za mwanzoni, sasa Huyu hapa duniani ndani ya watu Wake. Mwamini Yeye. Yeye yupo hapa.

²⁵¹ Kusudi tu mweze kumwona Yeye, (huenda kuna wageni), naomba Mungu wa Mbinguni aheshimu yale niliyosema kumhusu Yeye. Sasa nawatakeni ninyi kwenye wasikilizaji, tafadhali, mtu yeyote asitoke nje tena. Mpeni tu Mungu wa Mbinguni heshima kiasi hiki, kuketi tu kwa kitambo kidogo. Sasa msisogee. Hebu kila mtu humu ndani, aliye mgonjwa au mhitaji, inua mkono wako. Ama uwe... Vema. Asanteni. Sasa, sijui...

²⁵² Ninamjua Ndugu King, anayeketi moja kwa moja hapa. Ndio kwanza nimtambue, dakika chache tu zilizopita. Nina hakika. Nafikiri huyo ndiye, ni Ndugu King anayeketi hapo. Aliudhamini mkutano wangu uliopita hapa. Ndugu King, siwezi kusema kile ninachotaka kusema, bali unajua kuwa ninajua kile ninachotaka kusema. Umepitia kinoo, maskini ndugu yangu. Mungu akurehemu.

²⁵³ Wengine, sijui. Ningali ninamwona Pat Tyler ameketi hapa. Nafikiri huyo ndiye mwanaume pekee katika jengo, au mwanamke pekee, chochote nijuacho chochote, ni mwanamume huyu, Pat Tyler, aliyeketi hapa.

²⁵⁴ Aminini sasa. Na kama mimi ni mtumishi wa Mungu, na kama Mungu yupo hapa, nami nimelitambulisha Neno Lake

kuwa ni kweli; basi hebu Mungu wa Mbinguni, Yeye aliyemfufua Mwanawe, Yesu Kristo, ambaye alitoa ahadi hizi, alitambulishe pamoja nanyi, kwamba nimesema Kweli.

²⁵⁵ Angeifanya namna gani? Si kwa kuja huku amevaa joho, na ndevu. Bali Uhai Wake, “Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi.” Uhai ulioko ndani ya Mzabibu uko ndani ya tawi. “Kazi nizifanyazo Mimi mtazifanya pia,” na kuliahidi katika siku hii, wakati tawi jingine litakapochipuka. Tunayo matawi mengi sana yaliyopandikizwa; hakika, litazaa tunda, bali si tunda la aina hii. Loo, la.

²⁵⁶ Niliona mti fulani huko Phoenix, si muda mrefu uliopita, ulikuwa na yapata matunda manane au tisa mbali mbali juu yake. Ulikuwa ni wa Ndugu John Sharrit. Nikasema, “Ni mti wa aina gani huo?”

Akasema, “Ni mchungwa, Ndugu Branham.”

²⁵⁷ “Mbona,” nikasema, “kuna malimau na balungi na—na makangaja, na machenza.”

²⁵⁸ Naye akasema, “Naam, yote ni matunda ya jamii ya chungwa.” Kasema, “Niliipandikiza mle.”

²⁵⁹ “Loo,” nikasema, “Naona. Sasa, mwaka ujao, yote yatakuwa ni mchungwa?”

²⁶⁰ Akasema, “Loo, la. A-ha! La. Mwaka ujao li—limau litakuwa limau, ba—balungi itakuwa balungi.”

²⁶¹ Nikasema, “Kutokana na mzabibu uo huo? Kutokana na uo huo, kutoka kwa—kutoka kwa mchungwa?”

²⁶² Akasema, “Naam. Yote ni matunda jamii ya chungwa, Ndugu Branham. Yataishi kwa tunda la jamii ya chungwa.”

²⁶³ Ndipo nikahisi machozi yakitiririka mashavuni mwangu. Nikasema, “Bwana Yesu, ninajua unachomaanisha sasa.” Hicho hapo. Madhehebu haya yamejipandikiza yenyewe, bali yanazaa matunda ya kimadhehebu.

²⁶⁴ Sikilizeni. Ikiwa tawi hilo la asili litawahi kuzaa, Mzabibu halisi ukizaa tawi jingine, litakuwa la asili. Liaminini.

²⁶⁵ [Dada mmoja anaanza kunena katika lugha nyingine—Mh.] Sh-sh-sh-sh-sh! [Anaendelea na kumaliza. Ndugu fulani anatoa tafsiri.] Mshukuru Bwana. Jinsi alivyoahidi hilo!

²⁶⁶ Sasa kila mtu kuwa na kicho kabisa. Ninaenda kusimama tu hapa na kumwuliza Bwana Yesu.

²⁶⁷ Hii ni karama. Karama ni nini? Hata nikiweza kusongeza mawazo yangu mwenyewe, ninaweza kuufanya uhai wangu mwenyewe kutoka kwangu, u—uhai wangu wa kimaumbile, nafsi yangu, hiyo ni William Branham; ikiwa ninaweza kumwondoa njiani, Mungu ataitumia roho, mwili kunena.

268 Jalia Roho Mtakatifu aje sasa, Bwana, kusudi waweze kuona, kwa wanadamu, kwamba Roho Mtakatifu aliyetambulishwa yupo hapa. Karama kujiweka mwenyewe, jinsi . . .

Kila mtu awe na kicho kabisa. Kaeni kwa utulivu.

269 Mwanaume tu anayeketi hapa nje. Sasa ninawatakeni nyote mwinue vichwa vyenu na mwangalie kwa dakika moja. Mwaweza kuona Hiyo papa hapa juu ya mwanamume huyu? Nuru, Nuru ya kaharabu, ikiwaka, kuzunguka hii. Ni wangapi walioona picha Yake? Ilipigwa hapa Houston. Mnaona? Iko Washington, DC, kote ulimwenguni. Kiumbe pekee cha Kimbinguni kilichowahi kupigwa picha, katika ulimwengu mzima. Hii hapa papa hapa sasa.

270 Ninachukua kila roho humu ndani chini ya udhibiti wangu, katika Jina la Yesu Kristo.

271 Mwanamume huyu anaugua tatizo la tezi kwenye koo lake. Simjui, sijawahi kumwona maishani mwangu, bali huo ndio ukweli. Hiyo si ni kweli, bwana? Unaamini sasa? Mwanaume uliye huko nyuma, unaamini kwamba Mungu atanijulisha habari zako? Wewe ni Bw. Hall. Hilo ndilo jina lako, sivyo? Vema, bwana. Imekwisha sasa. Imani yako inakuponya.

272 Ningeweza kuitisha mstari wa maombi, na kuwaleta hapa juu jukwaani. Hakuna haja ya huo. Hebu tuchukue moja ya safu hizi hapa, mahali fulani. Hapa, anzeni papa hapa. Huyu hapa msichana mdogo ameketi hapa. Angalia huku, mpenzi. Huenda huna shida yoyote, sijui. Lakini sema tu, badala ya mstari wa maombi kuja hapa juu, hebu tuufanyize hapa chini.

273 Angalia hapa, mpenzi. Mwangelie Ndugu Branham. Katika siku ambazo Yesu alikuwa hapa duniani . . . Naam, yeye ni mgonjwa. Yeye ni mgonjwa sana, yule mtoto pale. Naam, bwana. Kama Yesu angalikuwa hapa, Yeye angeweza kukuambia shida yako, sivyo? Je! unaamini kwamba Yesu alimtuma Ndugu Branham kufanya hilo? Kama nikikwambia shida yako, unaamini kwamba Yeye atakuponya? Ni kisukari, mtoto huyo mdogo. Hakuna njia kwake kuponywa nje ya Mungu. Je! unaamini, kipeenzi?

274 Sasa mama huyo anayeketi karibu, aliyeinua mkono, huyo ndiye mamae mtoto huyo. Hiyo ni kweli. Weka mkono wako juu yake, dada. Amini sasa. Mungu alimleta mtoto huyo kwako. Mungu na ajalie uponyaji wake.

275 Mama huyu anayefuata, anayeketi karibu na huyo mama hapo. Angalia hapa nilipo, mama. Je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake, mtumishi wa Mungu? Ikiwa Mungu ataniambia jambo fulani maishani mwako, ama kile unachohitaji, kama wewe ni mgonjwa, ama si mgonjwa, ama chochote kile; kama Mungu ataniambia shauku zako, je! utaamini? Ama kitu kama hicho, sijui kile Yeye atachofanya, je! utaamini hilo? Unajua ingebidi iwe ni Yesu Kristo.

²⁷⁶ Uko mbali sana nami. Usingeweza kunigusa kama ilikupasa kufanya hivyo; maana, kama ungenigusa, ingekuwa ni jambo la kimwili. Inakubidi kugusa Roho. Roho ni Kristo. “Yeye ndiye Kuhani Mkuu sasa,” Biblia inasema, “aweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.”

²⁷⁷ Unasumbuka, pia. Je! unaamini Mungu anaweza kuniambia lililo tatizo lako? Unasumbuliwa na tatizo la mgongo, na shinikizo la damu, pia u—una shinikizo la juu la damu, tena una tatizo la moyo. Hiyo ni kweli kabisa. Ikiwa hiyo ni kweli, inua mkono wako. Hiyo ni kweli. Je! unaamini sasa?

²⁷⁸ Vipi kukuhusu wewe hapo uliyemkumbatia? Mama uliye upande huu, angalia hapa. Je! wewe... Mimi ni mgeni kwako. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Unaniamini, kwamba kile ambacho nimesema ni kweli, kwamba nimekuambia Kweli. Je! unaamini kwamba Mungu anaweza kunifunulia tatizo lako? Lolote, lolote lililo, unaamini Yeye angeweza kufunua hilo? Kwa kweli si jambo unalotaka liombewe. Unayo kadi ya maombi, ninaona mkononi mwako; wewe ndiwe wa kwanza aliye na kadi ya maombi. Je! unaamini Mungu anaweza kuniambia ni kwa nini una kadi ya maombi? Ni kwa ajili ya mume wako. Unaamini kwamba Mungu anaweza kuniambia shida ya mume wako? Mungu asipomgusa, atakufa. [Dada huyo anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Ana kansa na pia ana tatizo la pafu. Hiyo ni kweli, siyo? [“Hiyo ni kweli.”] A-ha. Inua mkono wako ikiwa ni hivyo. Kama utaamini, hao wengine wataamini, anaweza kuponywa.

²⁷⁹ Mwanamume huyo anayeketi karibu na wewe, unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake, bwana? Ikiwa Mungu anaweza kunifunulia lililo tatizo lako, hivi basi utaamini kwa moyo wako wote? Unasumbuliwa na tatizo la moyo. Hiyo ni kweli. Ikiwa hiyo ni kweli, inua mkono wako. A-ha. Vema.

²⁸⁰ Mama huyo ndio kwanza atikise kichwa na kujitikisa mwenyewe, namna hiyo, anayeketi karibu na wewe. Unaamini kwamba Mungu anaweza kuniambia kilicho moyo wako, ama kitu unachotamani moyoni mwako, au kitu fulani, ama kitu fulani, unachomwombea mtu mwingine? Unaamini Mungu angeweza kunifunulia wakati upako ukiwa hapa, nasi tunaweza kuuona na kuona kwamba Huo hauna budi kuwa kitu halisi? Unafunua siri za moyo, ukisema ni kitu gani, kama tu vile Yesu alivyomwambia yule mwanamke kisimani. Sasa wewe pia unateseka. Wewe, wewe unasumbuliwa na tatizo la mgongo. Lako liko mgongoni. Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. A-ha.

²⁸¹ Sasa huyo mama aliye karibu naye, unayelia, huku kibeti chako kikiwa mfukoni mwako, umevalia gauni ya bluu, nywele nyeusi, mnene. Niangalie mimi. Je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? Angalia hapa. Unaona, uko kwenye safu ya

mbele, ninaweza kuwasiliana nawe kwa urahisi, kwa msaada wa Mungu. Unaamini kwamba Mungu anaweza kuniambia kwamba tatizo lako ni nini, kama tu vile ungekuwa katika mstari wa maombi? Unaamini kuwa hiyo ingeweza kuwa hivyo, kutoka hapa? Unaamini? Una shinikizo kuu la damu linalokusumbua. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema. Wewe amini, na unaweza kuponywa.

²⁸² Mama huyo aliye karibu na yeye. Unawazia nini, dada? Angalia huku, niliko. Unaniamini kuwa ni nabii wa Mungu, au mtumishi Wake? Unaamini hilo, kwa moyo wako wote? Unaamini Mungu anaweza kunielezea, kama yule mwanamke kisimani, wakati mwanamke huyo na Yesu walipokutana, anayeweza kuniambia kilicho shida yako? Je! unaamini? Hiyo ingekusaidia, ingekusaidia kuamini? Angalia. Loo, una kitu cha hatari. Ni mwana, mvulana. A-ha. Naye mvulana huyo ana wasiwasi wa akili. Yuko nyumbani. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Amini kwa moyo wako wote, mvulana huyo atapona. Wewe amini.

²⁸³ Mama anayefuata hapo. Unaamini, dada, kwa moyo wako wote? Je! unaniamini kuwa ni nabii Wake, mtumishi Wake? Je! unaamini ni Yesu Kristo, kwa karama tu ambayo. . .

²⁸⁴ Kutabiri ni karama. Mnajua, karama ya Mungu, imekusudiwa huko nyuma kabla ulimwengu kuanza. Ilibidi ikusudiwe kwa ajili ya siku hii. Huna njia yoyote ya kujua nini ndiyo nini. Mungu huitambulisha tu na kufasiri Neno Lake.

²⁸⁵ Je! Mnaamini hilo kuwa ni kweli, lile mliilosikia? Mnaamini ningeweza. . . Kama ningeweza kukuambia kuwa shida ni nini, unajua isingeweza kuwa ni mimi. Ingebidi iwe ni Mwingine; sauti yangu tu, bali Mwingine akiitumia. Kama tu vile maikrofoni hii, ni bubu mpaka kitu fulani kizungumze kuipitia. Hatufahamiani. Unaona? Nilipoteza mwende- . . .

²⁸⁶ Huyu hapa. Naam, bwana. Mama huyo anaugua upungufu wa damu. Uko kwenye damu yake. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, mama. Hiyo ni kweli. Wewe, pia unamwomba jamaa huyu mdogo hapo mwisho. Huyu ni mwanao mdogo aliyeketi hapo mwisho. Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako. Kama Mungu anaweza kuniambia shida ya mwanao mdogo, je! utaamini kwa moyo wako wote kwamba Mungu huzungumza nami, na hiyo ni kweli? Yeye anasumbuliwa na wasiwasi uliokithiri. Hiyo ni kweli. Hiyo si ni kweli? Basi weka mkono wako juu yake, na uamini kwa moyo wako wote, naye atapona.

²⁸⁷ Nawapeni changamoto kuamini hilo! BWANA MUNGU ASEMA HIVI. Texas, mkifa katika dhambi, mnakufa bila ya damu yangu juu yenu. Kumbukeni, damu yenu haiko juu yangu. Huo hapo Ukweli! Huyu ni Yesu Kristo akitambulishwa, mistari ya maombi, popote pale. Mwaminini Bwana Yesu

Kristo! Je! mnaamini? Hivi mmeshawishika, mmeshawishika kabisa kwamba haina budi kuwa ni Yesu Kristo kulingana na Neno la ahadi ya siku hii? Inueni mikono yenu, kila mtu aliyeshawishika kabisa kwamba ni Bwana Yesu Kristo. Amina. Mungu awabariki.

²⁸⁸ Ninajua mmefunzwa. Mmefunzwa, kila mmoja wenu, jambo fulani. Nami ninaona ni—ni...kwa hiyo upako, unaweza tu kuivuta kila mahali sasa, mnaona. Mmefundishwa kwamba lazima mweke mikono juu ya wagonjwa. Hiyo ni desturi. Ni sawa. Yesu aliidhinisha.

²⁸⁹ Bali yule Mrumi, hicho ndicho nimekuwa nikijaribu kuwaleteni, juma hili. “Mimi sistahili,” kasema Mrumi, “hata uje chini ya paa langu. Sema tu Neno!” Mnaona?

²⁹⁰ Mtu akikuwekea mikono, basi, “Ndugu *Nanii* aliniwekea mikono, utukufu kwa Mungu!”

²⁹¹ Ni—ni—nitawaomba wahudumu, wahudumu wanaoamini waje hapa, kusudi isiwe tu ni mikono yangu. Ni—ni kile tu Yesu alichosema, “Wataweka mikono juu ya wagonjwa.”

²⁹² Tunaenda kuwaomba wagonjwa, kila mmoja. Ni wangapi walio na kadi za maombi, kote katika jengo, hapo hebu tuone mikono yenu. Naam, tuliwaahidi, sasa tuna nusu saa kutimiza hiyo. Nitauliza. . .

²⁹³ Tungeendesha huu namna gani, Ndugu Pearry. Je! una mashauri yoyote? Kutoka upande huu *hapa*?

²⁹⁴ Hebu safu *hii* hapa nje, walio na kadi za maombi, wasimame kuegemea ukuta, watokee *huko* na kusimama kuegemea ukuta. [Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham kuhusu mstari wa maombi—Mh.] Vema, bwana. Hiyo ni sawa. Simameni upande *ule*.

²⁹⁵ Wote kutoka katikati hapa, kutoka...sasa ninyi simameni kwenye marefu, mnaona. Ninyi simameni tu kwenye marefu, walio kwenye marefu haya, katikati hapa, simameni huko kwenye marefu.

²⁹⁶ Walioko upande *ule*, simameni upande *huo*. Walioko humu ndani, simameni hapa katikati, upande *huu*. Na walioko upande *ule*, simameni hapo ndani. Na mfuate tu mistari yenu inavyokuja. Hiyo ni kweli. Watakuwa huko chini kuwaelezea cha kufanya.

²⁹⁷ Ninauliza...Hii ni sawa, Ndugu Pearry? [Ndugu Pearry Green anasema, “Hakika.”—Mh.] Ninaomba wahudumu wanaomwamini Kristo, kwamba Kristo atawaponya watu hawa wagonjwa kwa kuweka mikono juu yao na kufuata amri Zake, ninawaombeni mje hapa na kusimama pamoja nami kama mnaamini hili kuwa ni Kweli. Mhudumu yeyote wa Injili, kama wewe ni Mmethodisti, Baptisti, Presbiteri, Lutheri, kasisi wa Katoliki, chochote ulicho; kama unaamini kuwa Yesu Kristo

huwaponya wagonjwa, na ameagiza wanafunzi Wake kuweka mikono juu ya wagonjwa, kwa ajili ya uponyaji wao, je! utakuja hapa?

²⁹⁸ [Ndugu fulani anasema, “Ambia kila mtu aende nyuma.” Ndugu Pearry Green anasema, “Naomba kila mtu anayetaka kuombewa, aende nyuma.”—Mh.]

²⁹⁹ Sasa nendeni nyuma na mzunguke, mnaona. Wote kwenye mistari hii sasa, nendeni moja kwa moja nyuma na mchukue mahali penu, mzunguke moja kwa moja upande *ule*, na kisha mrudi moja kwa moja mahali penu tena, kwa utaratibu tu iwezekanavyo.

³⁰⁰ Sijui, ndugu, hivi inafaa twende kule chini? Nafikiri hilo ni wazo jema. Sasa, heri niache maikrofoni hii hapa. Hebu... Roy, wewe simama hapa karibu na maikrofoni. Ama, naam, heri ushuke pamoja nami, unaona. Naam. Ama, isipokuwa uwe unataka kusimama hapa. Vema, Roy, wewe simama hapa basi. Vema.

³⁰¹ Sasa mnaenda. Sasa ninataka, mtu yeyote asiondoke, tafadhali. Mnaona, jambo lile lile ambalo tumekuwa tukiombea!

³⁰² Sasa mnasema, “Ndugu Branham, ni kwa nini uliwaleta wahudumu hawa wote hapa juu?” Nitakuja moja kwa moja pamoja nao. Bali mimi...

³⁰³ Mnaona, jambo ni kwamba, wana haki sawa kuwaombea wagonjwa kama nilivyo nayo, ama mtu yeyote alivyo nayo, kama vile Oral Roberts ama—ama kundi lolote la maaskofu, haijalishi ni nani. Wana haki ya kuombea wagonjwa kama tu vile Petro, Yakobo, Yohana, Mathayo, Marko, Luka, yeyote wa hao wengine walivyokuwa nayo. Wao ni wahudumu, walioitwa na Mungu. Nimeona ndugu wawili au watatu humo ndani ninaowajua, binafsi, walio na huduma ya kuwaombea wagonjwa.

³⁰⁴ Sasa wakati mkifanyiza mstari hapa juu, ninataka... Ni wangapi kwenye kusanyiko hili wameshawishika kabisa, kwa moyo wako wote, kwamba unaamini ni mapenzi ya Mungu kuwaponya watu hawa. [Kusanyiko linashangilia na kusema, “Amina.”—Mh.] Hakika, ndivyo. Kweli, ni mapenzi ya Mungu kuwaponya.

³⁰⁵ Sasa wanaponywa namna gani? Sasa, kama Yeye angalikuwa hapa, Mwenyewe, asingalifanya zaidi ya kile amefanya sasa hivi. Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kile tu alichofanya sasa, hicho ndicho angefanya, maana ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

³⁰⁶ Ni wangapi wanaojua kwamba Yohana Mtakatifu 5:19 inasema hili, “Mwana hawezi kufanya lolote Mwenyewe”? Ni wangapi wanajua hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] “Ila lile amwonalo Baba analifanya, hilo afanya Mwana.” Mnaamini hilo? [“Amina.”] Basi, Yesu kamwe hakutenda

mwujiza mmoja mpaka Baba alipomwonyesha, kwa ono, jambo la kufanya. Hilo ni Neno Lake Mwenyewe. Kama sivyo lilivyo, basi sote tumepotea, hatujui mahali tulipo. Haya basi. Mnaona, Maneno Yake hayakosei.

³⁰⁷ Mwangalie Yeye akipitia, birika la Bethesda, saa chache... yapata saa moja kabla ya hapo. Kulikuwa na umati mkubwa wa walemavu, vipofu, viwete, waliopooza. Ni wangapi wanajua hiyo ni kweli? Naye hakumgusa hata mmoja wao, hata hivyo alikuwa ni Mungu wa huruma. Mnaamini alikuwa na huruma? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Akimwacha yule mama, aliyekuwa na mtoto mwenye kichwa kilichojawa maji; yule maskini baba kipofu, akimwita mtu fulani, kumweka ndani ya maji yakitibuliwa. Mungu mwenye huruma! Mnaona?

³⁰⁸ Watu hawajui huruma ni kitu gani. Wanachanganya upendo wa *fileo* na Upendo wa Agape; ni namna mbili za upendo, kwa jumla. Huruma ni kitu kile kile; shauku, na huruma, ni tofauti.

³⁰⁹ Lakini, angalia, Yeye alimwendea mtu ambaye alikuwa labda na shida ya tezi kibofu, ama labda ilikuwa ni kifua kikuu. Ilikuwa imekawia; alikuwa amekuwa nayo kwa... ilikuwa— ilikuwa ni miaka thelathini na minane alikuwa amekuwa nayo. Haikuwa inaenda kumwua. Ndipo akamwendea mtu huyo, na Yeye akasema, "Je! wataka kuwa mzima?" Ni wangapi wanajua hiyo ni kweli? Akawaacha wasikilizaji wengine wote wakae hapo.

³¹⁰ Vipi kama angefanya hivyo huku Beaumont, leo hii? "Loo, jamani! Uponyaji wa Kiungu ni bure, basi, mnaona."

³¹¹ Mnaona, hawaelewi. Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele. "Sitendi lolote mpaka Baba anionyeshe kwanza."

³¹² Lakini watu wengi walikaa tu katika kivuli Chake, wakaponywa kwa imani yao wenyewe. Maskini mwanamke fulani aligusa vazi Lake akawa mzima. Ni wangapi wanajua hilo? Uponyaji unategemea imani yako. Utambulisho wa Mungu unategemea ahadi ya Neno Lake, lakini imani yako katika utambulisho Wake ndiyo inayokuponya. Usipoamini, haijalishi, mtu mtakatifu kuliko wote katika ulimwengu wote angeweza kusimama hapa na kuomba mchana kutwa, haitafaa kitu hata kidogo mpaka uamini, kabisa, wewe mwenyewe. Yesu huenda akasimama hapa Mwenyewe, katika mwili wa kibinadamu, akuwekee mikono, na bado usingaliponywa. Ni wangapi wanajua hilo? "Kazi nyingi kuu asingeweza kufanya kwa sababu ya kutokuamini kwao." Hilo ni Andiko.

³¹³ Kwa hiyo, mnaona, nyinyi katika mstari wa maombi, haina budi kuwa ni imani yako katika Neno. Sasa ukimwona Mungu akifanya kile alichofanya... Angalia, hebu nitoe tu ushuhuda mmoja mdogo wakati mkijiandaa. Sikilizeni kwa makini. Usiku wa kutangulia jana...

314 Yupo maskini mhudumu mmoja hapa mahali fulani. Nilimwona hapa, muda mfupi uliopita. Jina lake ni Martin. Nasahau. . . Yeye ni mmoja wa wadhamini. Papa *hapa*.

315 Yapata usiku wa manane, karibu hapo, mtu fulani aliniamsha katika chumba changu. Jamaa mdogo akilia, maskini mhudumu, mtoto wake mchanga alikuwa tu amefariki. Machozi yakitiririka usoni mwake.

316 Yuko ndani hapa mahali fulani katika. . . Ule mji wanakoishi unaitwaje? [Mtu fulani anasema, "Missouri."—Mh.] Missouri. Juu wapi? ["Wardell, Missouri."] Wardell, Missouri. Ninamjua mvulana huyo. Ninamjua ndugu yake hapa, pia. Hao ni rafiki zangu.

317 Ndugu huyu aliingia mle huku machozi yakitiririka mashavuni mwake, kasema, "Ndugu Branham, ndio kwanza niite. . . Ndio kwanza mke wangu aniite. Mtoto wangu mchanga alikoma tu kupumua." Akaweka mikono yake juu yangu, kasema, "Ndugu Branham, ninaamini Neno la Bwana liko pamoja nawe." Loo, Mungu angewezeje. . . Kama tu vile, "Hata sasa, Bwana! Kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa." Mnaona, hakuwa akikiri kwangu mimi. Alikuwa akikiri Neno la Bwana, mnaona, kwamba nilikuwa ninahubiri Ukweli. Akasema, "Ninaamini Neno la Bwana liko pamoja nawe. Mwombe tu Yeye; mtoto wangu atakuwa mzima." Katika dakika kumi kuanzia hapo, mtoto wake alikuwa akipumua kawaida, ni mzima sasa.

318 Mwanangu anayesimama hapa mahali fulani, Billy Paul, alikuwa ametoka ili kuzungumza naye. Nami nilikuwa hapo nimevaa pajama yangu. Na yapata dakika chache baadaye akarudi, kasema, "Baba, Baba, angalia hapa!" Nalo koo lake limevimba kabisa, na ni jekundu, na alama kubwa, alama karibu ukubwa huo kote. Kasema, "Buibui mkubwa mweusi aliye na doa jekundu! Nilikuwa nimesimama pale, nilikuwa nikizungumza na John, ndipo akaniuma pale. Basi angalia hapo, panafula."

319 Nikasema, "Loo, Billy, mjane mweusi, labda." Nami nikasema, "Angalia koo lako, jinsi lilivyofura."

320 Nikaweka mkono wangu pale, nikasema, "Bwana Yesu," katika dakika kumi kuanzia hapo hakukuwa hata na. . . hata usingetambua kwamba alama iliwahi kuwa hapo. Mnaona? Ni kitu gani? Mnaona?

321 Mtu fulani akaingia, hivi majuzi, na akasema, ofisini. Na mmoja wa maafisa akatoka nje. Ndipo akasema, "Mwambie Ndugu Branham aseme tu kuwa mtoto wangu. . ." Akasema, "Ninaamini kama. . . kile ungesema." Lakini, mnaona, siwezi kulisema mpaka Yeye aniambie.

322 Lakini hapa ninalo Neno linasema hivi, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya

wagonjwa, watapata afya.” Sasa, Mungu hawezi kufanya mambo hayo na kukuacha usimame hapo. Inakubidi kuamini. Wewe amini kitu hicho hicho, kitatendeka kwako. Bali huna budi kuamini, sio tu kujifanya. Huna budi kuamini hicho.

Sasa hebu tuombe, kwanza, sote pamoja.

³²³ Ninataka kila mmoja wenu nyote... huku ndugu hawa wakisimama hapa kwenye maikrofoni hii. Ninateremka huko chini kusudi niweze kuwawekea mikono, pia. Hao ni watu wangu, hao ni nanii wangu... Ni nyota katika taji yangu, vile vile walivyo kwa taji yako, enyi ndugu zangu wahudumu. Ninakuja hapo kwa sababu tunawapenda, nao ni watoto wa Mungu. Tunakuja ili kuwasaidia.

Sasa hebu na tuombe.

³²⁴ Bwana Yesu, mtu yule ambaye angeweza kusema kwamba Uwepo Wako haupo hapa, angeweza... kungekuwa na kitu fulani kasoro akilini. Kama vile tu mtu ambaye angekataa kukubali mwanga wa jua; mtu fulani amwambie jua linawaka, yeye angekimbia aingie chini kwenye orofa ya chini na kufunga mlango, na kusema, “Ninakataa tu kuamini hilo! Ninakataa kuamini hilo!” Vema, tungejua, Bwana, kwamba mtu huyo ana shida fulani akilini. Na vivyo hivyo na mtu ambaye angezifunga hisia zake za huruma, mbele za Nuru ya Neno la Yesu Kristo likidhihirishwa, angeweza kusema, “Siamini Hilo.” mtu huyo ana kasoro fulani kiroho.

³²⁵ Kwa hiyo tunajua kuwa Wewe upo hapa, Baba. Bila shaka lolote, tunaamini hilo. Tunaona nyayo Za—Zako. Tunaona ishara Zako. Tunaliona Neno Lako.

³²⁶ Wapo mamia wanaosimama hapa katika mstari huu wa maombi. Na watu wazuri wa Mungu wamesimama hapa, askari mashuhuri wa Imani; ninashuka chini ili kuweka bega langu pamoja na yao, Bwana. Wakati wagonjwa hawa watakopopitia kwenye mstari huu wa maombi, jalia kila mmoja wao ajue kwamba si kupitia tu karibu na watu fulani. Wanakuja chini ya Msalaba wa ahadi. Jalia watoke hapa wakiwa wamepona, waende wakishangilia, wapate afya; wamwambie mchungaji wao. Jalia hilo lisababishe kuanza kwa uamsho wa mtindo wa kale, kote chini katika nchi hizi, Bwana, ulete nafsi nyingi Kwako. Bwana, hao ni Wako. Wasaidie. Waponye, ninaomba, katika Jina la Yesu Kristo.

Ninataka kila mmoja sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, mkiomba.

³²⁷ Nami ninataka, wakati nyinyi... Sikilizeni, mstari wa maombi sasa. Unapopita, kama tu ambavyo ungekuwa chini ya Msalaba, amini kwa kila kitu kilichoko ndani yako. Nenda kutoka hapa ukishangilia, mwenye furaha, ukisema, “Asante, Bwana. Ninaamini uponyaji wangu.” Na iwapo huamini huo, basi ni afadhali uketi, kwa sababu haitakufaa hata kidogo.

³²⁸ Ninataka kusanyiko lote, kila mtu, kupenya hadi Mbinguni namna hiyo, katika Uwepo wa Kristo, “Bwana Yesu, jitambulisha Mwenyewe kwetu sasa! Waponye hawa wagonjwa!” Mtafanya hivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Ndugu Borders, huku ukiimba, *Amini Tu*.

³²⁹ Iache hiyo hapa. Hatuihitaji. [Ndugu fulani anauliza kuhusu maikrofoni, “Utaiacha hapa?”—Mh.] Naam.

³³⁰ [Ndugu Branham na wahudumu wanashuka sasa na kuombea kila mtu anayekuja kupitia mstari wa maombi, huku Ndugu Roy Borders akiongoza kusanyiko katika kuimba *Amini Tu*. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

³³¹ Amini tu! Hebu tuinue mikono yetu sasa.

Mambo yote yanawezekana, amini tu.

Sasa hebu tuliseme namna hii:

Sasa naamini, loo, sasa naamini,
Mambo yote yanawezekana, sasa naamini,
Sasa naamini, loo, sasa naamini,
Mambo yote yanawezekana, loo, sasa naamini.

³³² Hata nitakapowaona tena, ninataka kuondoka Texas nikiwaona wakitangaza kwa sauti kuu sifa za Mungu. Hebu na tuinue tu mikono yetu na kumpa Mungu sifa, kila mmoja wetu. [Kusanyiko kwa furaha linapaza sauti na kumsifu Mungu—Mh.]

³³³ Bwana Yesu, tunakushukuru kwa ajili ya Neno Lako, kile ambacho umetufanyia. Ninakushukuru, kwa ajili ya kuweza kuzungumzia watu hawa wazuri, na kuona uweza Wako na baraka juu yao. Wabariki, Bwana. Jalia waelewe. Pia jalia Roho Mtakatifu amponye kila mmoja na kumwokoa kila mmoja, katika siku hizi za mwisho. Kupitia Jina la Yesu Kristo, Bwana, ninawakabidhi Kwako kwa ajili ya malighafi kwa ajili ya Bibi-arusi, kwa kuwa wanaamini kupitia neema ya Mungu. 

USHAWISHI SWA64-0315

(Influence)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili alasiri, tarehe 15 Machi, 1964, katika Ukumbi Wa Manispaa kule Beaumont, Texas, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org